# *Utuonyeshe Baba*

Na tuendelee kusimama na kuinamisha tu vichwa vyetu kwa muda mfupi kwa ajili ya maombi. Mambo ya kwanza kwanza, bila shaka, ni kukutana na Mungu. Sijui usiku wa leo kama kuna haja zozote maalum miongoni mwetu, ambazo mngetaka Mungu ajibu usiku wa leo, kama utaacha tu ijulikane kwa mkono wako ulioinuliwa Kwake. Kumbuka tu moyoni mwako kile unachotaka, na umwombe Baba sasa tunapoomba.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tumekusanyika katika Jina la Mwana Wako mpendwa, Bwana Yesu. Tunatambua uchaji wa majira haya. Yakiisha kupita yatakuwa ni historia, nasi tutatoa hesabu, kwenye Siku ya Hukumu, kwa ajili ya kuwa hapa usiku wa leo, na kwa yale tufanyayo. Hivyo basi, Baba, tunakuja Kwako na vichwa vilivyoinamishwa na mioyo iliyoinamishwa, na tukiomba rehema, na kwamba Ro—Roho Mtakatifu mkuu aweze kuja juu yetu na kutuongoza kwa yale tunayopaswa kusema na yale tunayopaswa kufanya.

3 Tunaomba, Baba, kwa ajili ya kila mmoja aliyeinua mkono. Wewe unajua ni nini kilichokuwa chini ya mkono huo, haja. Na sisi tunaleta haja zetu sasa mbele ya Kiti Chako kikuu cha Enzi cha pembe ya ndovu, ambapo ile Dhabihu imewekwa, Bwana Yesu, pamoja na hakikisho hili ambalo Yeye alituambia, "Kama tukimwomba Baba lolote katika Jina Lake, litatimizwa." Baba, tunaomba ya kwamba kila mmoja aliyeinua mkono wao atapokea haja yao usiku wa leo.

4 Bariki wale walio wagonjwa na wanaoteseka, Bwana. Jalia Roho Mtakatifu aje usiku wa leo, ajidhihirishe Mwenyewe, halisi sana, hata watu hawatakosa kumwona.

5 Tunawaombea wale ambao hawajaokoka, wasiojua msamaha wa dhambi, na wangali huko nje wakitangatanga gizani, bila tumaini, bila Mungu, wamepotea. Jalia nuru ya Injili, Injili tukufu ya Mwana wa Mungu, iwaangazie usiku wa leo, pia jalia mioyo yao iwe na njaa sana hata watamkubali Yeye kama Mwokozi wao. Tujalie, Baba. Tunaomba baraka hizi katika Jina la Bwana Yesu, Mwana Wako na Mwokozi wetu. Amina.

Mwaweza kuketi.

6 Daima ninayahesabu kuwa ni majaliwa kuwa katika... jukwaani, kuwazungumzia watu. Nilikuwa na furaha sana leo kusikia matokeo ya ule mkutano jana jioni, na wakati nikisikiliza kanda za jana jioni, jinsi ambavyo Roho Mtakatifu miongoni mwetu, yale aliyotutendea jana jioni. Shida pekee ninayopata na mkutano, ni kwamba hatuna muda mrefu wa kutosha kukaa. Usiku wa kesho tu ndio kufungwa kwa

mfululuzo huu. Na kuna yapata wawili tu wa ndugu wahudumu ambao hata nimekuwa na majaliwa ya kutambulishwa kwao, hata hivyo, wafadhili wa mkutano huu.

7 Na wengi wenu watu wazuri sijawahi kukutana nanyi maishani mwangu, na hakika ningetaka kupata fursa ya kwenda nyumbani pamoja nanyi Jumapili, kwa ajili chakula cha kutwa. Ninajua unaye mpishi aliye bora kuliko wote nchini. Na kwa hiyo, sisi, hakika ningetaka kufanya hivyo.

8 Lakini tunaondoka mara moja sasa, kuelekea. . .kwenda katika kazi ya Bwana. Labda, wetu unaofuata, baada ya kuondoka Arkansas, utakuwa huko juu Alaska. Kisha najisikia ya kwamba huenda Bwana anatuita twende nchi za ng'ambo mara moja, tena, kurudi Afrika.

9 Kwa hiyo imekuwa ni majaliwa makubwa sana, na mara ya kwanza kuwa hapa miongoni mwenu, na kuona imani hiyo kubwa ya kuitikia mliyo nayo, na, hata hivyo, huduma ni mpya kwenu. Ninajua ya kwamba m—mkutano mrefu zaidi kidogo ungefanya mambo makuu. Kwanza, mwajua, unahudhuria siku chache usiku, na kwa namna fulani unachukua maoni yako juu ya mwinjilisti huyo. Halafu basi, baada ya kitambo kidogo, ndipo ninii vyote. . .vile tungeviita vivuli, vinaondoka, tunaondolea mbali hofu zote, na kuona kwamba ni Injili, na Neno la Mungu, na Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Na hasa, tunapokuwa na mkutano kama huu ambapo watu wote wa imani zote wamealikwa, una makundi yaliyochanganyikana. Lakini, hata hivyo, tunamtumikia Mungu mmoja wa kweli na aliye hai, na kwa hiyo nina furaha sana kwa ajili ya hilo.

10 Sasa, kwa kawaida mimi hujaribu kuahidi kuwaachilia mwondoke mapema, na mimi nimeshindwa kila usiku. Lakini hizi ni nyakati ndogo fupi. Wakati mwingine, huko nyumbani, niko jukwaani kwa saa sita, nane, ama kumi. Kwa hiyo ninajua msingeweza kuvumilia hilo. Mna neema nyingi kukaa saa hii, saa moja na nusu. Bwana na awabariki sasa. Na—na mniombee, usiku wa leo, ninapojaribu kuzungumza kutoka kwenye fungu dogo hapa, na Maandiko fulani niliyoandika kwenye padi ya karatasi. Ambayo ningetaka kuyarejea, kwa dakika chache, na ndipo tutaona yale Bwana atatutaka tufanye.

11 Mwajua, kwa kweli, hatujui kile hasa Yeye atafanya, kwa sababu wana wa Mungu huongozwa na Roho wa Mungu. Inatupasa tu kuangalia na kukumbuka lolote Yeye atuambialo tufanye, basi tulifanye.

Kwa hiyo msisahau kesho usiku, usiku wa mwisho wa mkutano.

12 Halafu kiamshakinywa cha Wafanyabiashara wa Full Gospel ni Jumamosi asubuhi, kweli, ninaamini, katika chumba kiki hiki. Hiyo ni kweli? Hapa katika chumba hiki hiki. Na ninaamini mnaweza kupata tikiti kwenye dawati. Ama. . .Kwenye dawati.

Na bila shaka tutafurahi kuwa nanyi. Bwana akipenda, ninataka kuzungumza a—asubuhi hiyo, mara baada ya kiamshakinywa. Kama unaweza kuja na kupata kiamshakinywa pamoja nasi, tutafurahi ukifanya hivyo. Kama huwezi, vema, basi shuka uje kwa ajili ya Ujumbe mara baada ya kiamshakinywa, nasi tutafurahia wewe kuwa hapa. Nami ninataka kwa namna fulani kuchukua Ujumbe wa aina ya kiinjilisti kwa ajili ya huo.

13 Huu, nimejaribu kuutumia kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa, na uponyaji. Na sisi kwa namna fulani kwa njia ndogo. . . Si kwa hoja zozote za mafundisho, bali ili tu kuonyesha kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kwamba Yeye hajabadilika.

14 Na kwangu mimi, Hiyo, Biblia ama ni Neno la Mungu, au si Neno la Mungu. Ni—ni—ninaamini ya kwamba chochote ama ni sahihi au si sahihi. Huwezi kuwa nusu katikati. Hakuna Wakristo wazuri wa kupendeza. Umesikia tamshi hilo, bali hakuna kitu kama hicho. Ama wewe ni Mkristo au si Mkristo.

15 Na njia pekee unayoweza kuwa Mkristo, ni kuzaliwa tena kwa Roho wa Mungu. Hiyo ndiyo suluhisho pekee: chini ya Damu ya Bwana Yesu. Na wakati unapoungama dhambi zako kwa Mungu, na kweli una msamaha kutoka kwa Mungu, basi wewe si mwenye dhambi. Yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi. Akizitenda, ni bila kukusudia. "Mwabuduo akiisha kusafishwa mara moja asingejiona tena kuwa ana dhambi." Kwa mfano, katika Agano la Kale damu ya mafahali na mbuzi ilifunika tu dhambi; haikuiondoa. Bali Damu ya Yesu huiondoa. Inaitaliki. Haipo tena.

16 Kwa mfano, mama yangu, ndio kwanza tu aende Mbinguni, miezi michache iliyopita. Nilikuwa nimesimama karibu naye wakati alipoondoka, naye alifikia ambapo asingeweza kuzungumza. Nikasema, "Mama, ikiwa ungali unaweza kunisikia, kama Yesu angali ni mtamu kwako wakati unakufa, kadiri Yeye alivyokuwa wakati ulipokuwa hai, na mikutanoni; iwapo huwezi kuzungumza, pepesa tu macho yako upesi sana, nitajua unasema 'Ndiyo.'" Naye angeyapepesa macho yake, machozi yakitiririka tu usoni mwake. Ndipo akaenda kukutana na Bwana. Nami nilimbatiza mama yangu mwenyewe yapata miaka thelathini iliyopita. Nilikuwa tu maskini mvulana mhubiri.

17 Sasa, sasa, wakati angejaribu kutoa doa kwenye shati langu nilipokuwa mvulana mdogo, miaka mingi iliyopita, alikuwa akijaribu kupata mafuta ya makaa au—au kitu fulani na kuondoa hilo doa. Na kwa kweli, kamwe hakuliondoa doa hilo; alilifanya tu kubwa kidogo. Halikuonekana sana mahali pamoja. Lakini hivyo ndivyo, hayo ndiyo yote waliyokuwa nayo ya kutumia.

18 Sasa hebu tulinganishe hiyo na damu ya mbuzi na kondoo, kwa ajili ya dhambi. Ilikuwa tu ni. . . Ilikuwa ni upatanisho, hakika, bali haikufanya kazi vya kutosha, kwa sababu ilikuwa ni damu ya mnyama. Basi chembe hiyo ya damu inapovunjwa, ya asiye na hatia, mnaona, uhai wa mwana-kondoo usingeweza kumrudia mwanadamu, kwa sababu hakuwa na nafsi. Ni mnyama tu.

19 Bali wakati Yesu alipokuja na hiyo chembe ya Damu ikavunjwa, Uzima wa Mungu Mwenyewe unakuja juu yetu. Na sisi ni wana na binti za Mungu, pamoja na asili Yake. Angalieni.

20 Sasa, siku hizi, nikipata doa kwenye shati langu, mke wangu mpendwa, yeye huenda tu na kuchukua baadhi ya hizi hapa, nafikiri anaziita sabuni ya Kloroksi. Anaitia mle na yote yamekwisha.

21 Hebu tutafakari juu ya to—tone dogo tu la wino, tone moja dogo la wino mweusi. Sasa, wino huo ulitengenezwa kwa sababu fulani.

22 Na ni rangi. Na kweli kuna rangi moja tu; zingine zote zimetokana nayo; na rangi hiyo ni nyeupe. Lakini sasa, rangi hii, sijui kemikali za hii, lakini hebu tuseme hivi, ya kwamba ilibidi ianzie kwenye uumbaji, kwa sababu hivyo ndivyo ilivyo. Ilibidi itengenezwe na Muumba fulani. Muumba hana budi kuumba kiumbe.

23 Nalo tone hili dogo la wino, sasa, limeshuka, tuseme, kwa mfano, ni kwa kusudi fulani. Sasa hilo tone dogo la wino linaweza kuandika Yohana 3:16 na kusamehe dhambi zangu. Ama, tone hilo dogo la wino linaweza kuandika hukumu yangu ya kifo, kunituma kwenye—kwenye kinyongeo. Ni kwa kusudi fulani.

24 Lakini labda kama tone hilo dogo la wino, sasa, pamoja na rangi yake yote iliyo ndani yake, likianguka kwenye beseni ya sabuni, ni nini inafanyikia rangi hiyo? Sasa wazia tu, ni nini iliifanyikia? Kamwe hutaipata tena. Maji yaliyokuwa kwenye hiyo rangi, fo—fomula ya $H_2O$, yangali kwenye sabuni hiyo. Ni maji yanabadilika yakawa kitu gani chake? Lakini hebu tuseme kama rangi hiyo ilianza hapo mwanzo, inarudi, labda, ikawa kitu kama ukungu, ama gesi.

25 Nayo gesi hiyo, sasa, hii siyo fomula yake, ikitokea kuna mtu hapa anayefahamu hili. Ninasema tu hilo ili kwamba mjue kile ninachozungumzia.

26 Tuseme kulikuwa, ilirudi ikawa atomu, ama molekuli, kisha molekuli zikageuka kuwa atomu. Basi tuseme molekuli nne-sita-tisa kuongeza sita-tisa-saba zilifanya nyeusi. Kama ilikuwa sita-tisa-sita, ingetokea kuwa waridi, na kadhalika, na kuendelea ikarejea kwenye atomu. Kitu fulani ilibidi kuiamulia hapo mwanzo, kile ilikuwa inaenda kuwa.

27 Lakini mara inapoanguka kwenye sabuni hii hapa, inarudi moja kwa moja kupitia kila molekuli, kila atomu, ikamrudia Muumba wake.

28 Vema, hiyo ni kama dhambi zetu nyeusi. Mara zinapoungamwa katika Damu ya Yesu Kristo, zinasahaulika. Hamna dhambi tena, hata kidogo. Wewe ni huru na dhambi, na hamna dhambi kwake. Sio kwa sababu u—unastahili hilo, bali kwa sababu neema ya Mungu, hata umekuwa hivyo. Mwanadamu alipotenda dhambi, alivuka shimo kubwa kati yake na Mungu, na, kuacha, hakuna njia ya kurudi. Lakini, Mungu alikuwa mwingi wa rehema, a—akachukua kibadala. Naye mwana-kondoo alikuwa ndiye kibadala hicho kufikia utimilifu wa wakati, hapo Yeye, Mungu, alipofanyika mwili, kuondoa dhambi. Na sasa hata hakuna shimo pale, katikati. Mwanadamu na Mungu wakawa Baba na mwana. Hakuna dhambi, hata kidogo. Yeye huziweka katika bahari ya sabuni ya usahaulifu, na hata hawezi kuzikumbuka tena.

29 Sasa, sisi hatuwezi kufanya hivyo. Sisi ni wanadamu. Tunaweza kusamehe, bali hatuwezi kusahau. Lakini Mungu hana kikomo, na Yeye ni mkuu sana hata anaweza kusahau kabisa kwamba uliitenda. Wazia hilo. Hata hukuwahi kutenda dhambi. Basi hapo linamweka mwanadamu tena katika Uwepo wa Mungu kama Baba yake, na wewe ni mtoto Wake. Sisi ni wana na binti za Mungu sasa, si tutakuwa, sasa sisi ni wana na binti za Mungu. Loo, jamani! Hilo linawafanya Wamethodisti wajisikie kupaza sauti. Sivyo?

30 Sasa, tuna furaha sana kujua ya kwamba tunayo hii sabuni mashuhuri, mashuhuri mno ambayo Yesu Kristo alituletea, Damu Yake Mwenyewe. Tunaenda kuzungumza kidogo kumhusu Yeye sasa, kukupa nafasi ya kutulia angalau.

31 Na sasa hebu na tuyageukie Maandiko mkiweza, kwenye Yohana Mtakatifu, mlango wa 14 wa Yohana Mtakatifu. Ninataka kusoma vifungu vichache tu, kifungu cha 7 na cha 8, Yesu akizungumza.

> *Kama mngalinijua mimi,* ninyi *mngalimjua na Baba; na tangu sasa* ninyi *mnamjua, tena mmemwona.*
>
> *Filipo akamwambia, Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha.*

32 Ni—nitachukua somo la: *Utuonyeshe Baba.* Na—nataka kulizungumzia.

33 Basi moyo wa mwanadamu daima umetamani kumwona Mungu. Kama tulivyokuwa tukizungumza hivi majuzi usiku, juu ya wale Wayunani waliokuja kwenye ibada, nao wakasema, "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Walikuwa wamesikia habari Zake na wasingeweza kutulia mpaka wamemwona Yeye. Na mimi nafikiri hiyo kwa kweli ndiyo njia ambayo mwaminio halisi, wa kweli anayesikia habari za Mungu, kuna

kitu fulani ndani yake kinachodundadunda kwake kwamba laiti angalimwona Yeye.

34 Na, hata hivyo, tunaweza kumwona. Yesu alisema hapa, "Mkiniona Mimi, mmemwona Baba." Kwa hiyo tunajua ya kwamba unaweza kumwona. Sasa, kadiri tunavyoweza kufikiria juu ya wanadamu, daima wametamani kumwona Mungu.

35 Hata, Ayubu, nafikiri hicho ndicho kitabu cha kale kuliko vyote katika Biblia. Kinadhaniwa kuwa. Na kweli kiliandikwa kabla ya Musa kuandika Mwanzo. Basi Ayubu, yule mzee mashuhuri, na akimjua Mungu, basi alipofikia mahali ambapo aliingia katika taabu.

36 Kwa kawaida, mwanadamu atamtafuta Mungu anapokuwa katika shida. Nimewasikia watu wakisema, "Hata siamini kuna Mungu." Lakini acha aanguke na kujiumiza, ama daktari aseme anakaribia kufa, ndipo unamsikia akisema, "Ee Mungu," kama Bob Ingersoll. Wewe, utamwazia Mungu kabla hujamwazia mama yako ama yeyote yule, maana kuna kitu fulani tu ndani yako. Wewe ni mwanadamu.

37 Sasa tunaona ya kwamba Ayubu aliingia katika dhiki kubwa, hapo alipougua majipu na matatizo, na akaketi kwenye lundo la majivu na kuyakwaruza majipu yake.

38 Ninakumbuka nikichukua kitabu cha Ayubu, huko maskanini, miaka kadhaa iliyopita, na nilidumu karibu mwaka mzima kwenye kitabu cha Ayubu. Basi dada mmoja alikuwa na neema ya kutosha, hata hakuniuliza moja kwa moja jukwaani, bali aliniandikia barua. Akasema, "Ndugu Branham, ni lini utamwondoa Ayubu kwenye lundo hilo la majivu?" Nilimwacha ameketi pale nje, bali nilikuwa nikijaribu kujenga, kote, kujenga hoja mahali fulani, ule u—upeo wa hoja, ambao ungewaonyesha watu, ambapo tungefanya wito wa madhabahuni. Ndipo basi mamia wakaitikia.

39 Sasa, akiketi katika mateso, naye alikuwa na shauku ya kumwona Mungu. Akasema, "Laiti ningalijua mahali alipoishi, laiti ningalienda na kuubisha mlango Wake, ningeniii—ningemfahamu. Ningetaka kuketi chini na kuzungumza na Yeye." Mnaona, moyo wa mwanadamu ukimwita Mungu.

40 Na hakika, kama kuna shauku ya mwanadamu katika moyo wa binadamu, ambaye ni kiumbe cha Mungu, akimwita Mungu, hapana budi pawe na Mungu mahali fulani kujibu wito huo. Lakini wakati kilindi kinapokiita Kilindi, wito huo hauna budi kuitikiwa. Kabla kilindi hakijakuwapo *hapa* ndani, kikiita, hapana budi pawe na Kilindi huko nje, kuitikia wito huo, la sivyo kusingekuwako na wito *hapa* ndani.

41 Kama ambavyo nimesema mara nyingi, kabla hapajakuwapo na pezi mgongoni mwa samaki, ilibidi pawe na maji, kwanza, apate kutumia pezi hiyo, la sivyo asingekuwa na pezi yoyote. Kabla hapajakuwapo na mti kukua ardhini, ilibidi pawe na

ardhi, kwanza, la sivyo kusingekuwako na mti wowote. Na mradi tu kuna kiumbe, kuna Muumba wa kukiumba kiumbe hicho. Mnaona ninalomaanisha?

42 Na wakati kukiwa na njaa na kiu katika moyo wa mwanadamu, kwa ajili ya kitu fulani, hapana budi pawe na kitu cha kukiitikia, la sivyo kiu hakingekuwapo. Kwa hiyo, usiku wa leo, tupo hapa, tukisema, "Utuonyeshe Baba, latutosha." Na sasa, kama kuna Mungu, ambaye tunajua yuko, na wito moyoni mwetu kumwona, basi kwa nini hatuwezi kumwona? Kama kuna wito hapa unaotwambia tunataka kumwona Yeye, hapana budi pawe na sababu fulani ambayo sisi . . . njia fulani ya kumwona.

43 Na sasa mimi, kwa msaada wa Mungu, nitajaribu ku—kuwaonyesha, ama kuzungumza juu ya njia tatu mbalimbali, ama nitasema, njia nne mbalimbali, za kumwona Mungu. Nitazungumza juu ya: Mungu katika ulimwengu Wake; Mungu katika Neno Lake; Mungu katika Mwana Wake; Mungu katika watu Wake.

44 Na kwanza, sasa, tutazungumza juu ya Mungu katika ulimwengu Wake. Siamini ya kwamba mtu yeyote ambaye angeweza kuelewa jinsi ulimwengu huu unavyotenda kazi, jinsi ambavyo ule mfumo mkuu wa jua, na awe na akili timamu, angeweza kusema hakuna Mungu. Hivi mlijua dunia hii inazunguka, zaidi ya maili elfu moja kwa saa? Ni maili elfu ishirini na tano kuuzunguka. Inazunguka, hufanya mzunguko wake mkamilifu, kila saa ishirini na nne, kwa hiyo hiyo inaifanya kuenda zaidi ya maili elfu moja kwa saa *hivi*. Na wakati ikizunguka kwenye mzingo wa jua, sijui ni maili elfu ngapi kwa saa inaenda, na ni kamilifu sana katika wakati, haiukosi hata sekunde moja. Hakuna saa ya mkono, hakuna mtambo unaoweza kuwekwa katika ukamilifu wa namna hiyo, kuuzuia usichakae, ama hakuna saa ya mkono.

45 Nina saa ya mkono niliyopewa huko Uswisi, ambayo walisema, katika hela za Marekani, ingegharimu dola mia tatu kama ningaliinunua, moja ya saa zao zilizo nzuri sana. Hata hivyo, hiyo saa itapoteza, kila . . . dakika moja, mara kwa mara, ama kuongezea, ama—ama kitu fulani. Si—si ninii . . . Haiwezi kuwa kamilifu.

46 Na hata hivyo, angani, dunia hii hujizungusha kote. Ni nani anayeizungusha na kuiweka katika wakati huo mkamilifu? Hakika ingekuwa ikipunguza mwendo kidogo, kama kusingekuwapo na kitu fulani kinachoifanya iendelee kuzunguka. Basi unawezaje kuifanya izunguke kikamilifu hivi? Na inalizungukaje ju—ju—jua, jinsi inavyofanya, kikamilifu hivi? Na kufanya majira ya baridi kali, kiangazi, na kadhalika, kikamilifu tu kama ilivyo. Halafu hakuna mtu . . . Miaka elfu sita, haijapoteza sekunde moja; daima kwenye wakati. Ni kamilifu sana hata wanaweza kuweka wakati wa kupatwa kwa

jua na mwezi, sana, katika umbali wa miaka ishirini, wanaweza kukwambia saa kamili itakapopita, wakisoma falaki, wakisoma mfumo wa jua.

47 Ni kuu jinsi gani! Jamani, nafikiri, kama mtu angeweza kuangalia juu angani, ungeweza kulia kama yule mtunzi wa Kiswidi wa ule wimbo, *Jinsi Wewe Ulivyo Mkuu*, "Jinsi Wewe ulivyo mkuu!" Kuona hizo nyota ndogo, na labda haionekani kana kwamba zinaachana kwa inchi nne, angani, na hata hivyo ziko mbali sana moja na nyingine kuliko tulivyo mbali nazo. Na, hata hivyo, Mungu anatawala zote.

48 Na huko nje kwenye Mlima Wilson, California, kwa... Mnajimu aliyekuwa kwenye mkutano wangu, huko Chattanooga, alinipa ruhusa, pamoja na mnajimu huyu mwingine, kupanda kwenda kule juu na kuangalia darubini hii kuu. Walikuwa na picha, maana nilienda mchana. Nawe unaweza kuona maili milioni mia moja na ishirini ya nuru ya anga. Vunja hizo katika maili, nawe utaandika safu ya tisa-tisa kuizunguka Tucson mara kadhaa, ukijaribu kuzivunja katika maili.

49 Huwezi kulielewa akilini mwako: maili milioni mia moja na ishirini ya nuru ya anga, na kupita hapo ni miezi, nyota, na ulimwengu. Naye Baba yetu aliviumba, kwa mapenzi Yake mwenyewe, na kila kitu kikifanya kazi kikamilifu kabisa. Loo, ni ajabu vipi kuona jinsi Yeye alivyo mkuu, halafu jinsi anavyoweza kujifanya Mwenyewe rahisi, ili kwamba huta—hutaikosa njia.

50 Isaya 35 ilisema, "Wajapokuwa, wajinga hawatakosea mle." Haihitaji werevu, elimu. Ingalihitaji, mimi ndiye ningepotea. Inahitaji tu imani, kuliamini. Sio kujaribu kulielewa, bali kuliamini. Kwamba tu, Mungu aliifanya, na hilo latosha.

51 Sasa, tunaona ya kwamba watu wanajaribu kubishana kwamba sivyo ilivyo: makafiri. Hapa wakati fulani uliopita katika Colorado...Loo, nadhani imekuwa miaka thelathini, arobaini iliyopita. Kulikuwa na ka—kafiri alikuwa amepitia nchini, akijaribu kufanya watu wageukie ukafiri. Na hata akamwambia mama yake mwenyewe, alipokuwa yuafa.

Kasema, "Unaweza kunipa nini sasa?"

52 Akasema, "Ma, tabasamu na uyavumilie." Na ni jambo la jinsi gani kumwambia mama yako mwenyewe.

53 Akashikwa na fadhaa, kwa hiyo akaenda Magharibi, ku—kustarehe kidogo. Ndipo akafunga virago na kurudi milimani. Basi siku moja alikuwa akitembea huko...

54 Nao wahudumu waliogopa kumshambulia, walisema, kwa sababu alikuwa, loo, alikuwa mwerevu sana, mwenye elimu nyingi, mwanachuoni hodari. Basi wakaachana tu naye, wakamwacha apambane na akili zake.

55 Kwa hiyo basi, siku moja, walisema alienda kutembea na akatoka nje, na akaanza kuangalia miamba. Akaanza kushangaa, kweli, ilitoka wapi? Na muda si muda wajua, upepo ukaanza kuvuma kupitia kwenye misonobari, "Adamu, uko wapi?"

56 Mnaona, Biblia ilisema, "Wakinyamaza, mara moja mawe haya yatapiga kelele."

57 Kafiri huyu akaanguka magotini mwake akawa Mkristo mzuri, mwenye upendo, kwa sababu Mungu, katika ulimwengu Wake, aliita, kwamba, "Mimi ndimi Muumba Yule aliyeumba mbingu na nchi."

58 Wakati fulani uliopita, rafiki yangu, Bw. Wood, anaishi Jeffersonville, jirani yangu. Bw. Borders hapa, mmoja wa. . . meneja wangu, ameketi hapa usiku wa leo, anamfahamu vizuri. Alikuwa amehudhuria mkutano wa Louisville. Naye alikuwa ni Shahidi wa Yehova, na alikatazwa hata kuhudhuria mikutano hiyo, lakini alikuja na mke wake. Mke wake alikuwa ni mfuasi wa Church of God la Anderson.

59 Nao walimwona msichana mdogo pale, ameletwa jukwaani, na jinsi Roho Mtakatifu alivyomwambia msichana huyo mdogo shida yake ilikuwa ni nini, na ni muda gani alikuwa nao, akigeukia. . .ninasahau jina la ugonjwa huo, unaowageuza wakawa chokaa, ama jiwe. Hakuwa amesogea kwa yapata miaka mitatu. Ndipo kamwambia, katika Jina la Bwana, kwamba angepona. Basi kesho yake, msichana huyo alikimbia huku na huku kwenye vipandio; alikuwa jengoni usiku huo, akikimbia tu kote jukwaani, na kila kitu.

60 Bw. Wood, akiwa kidogo amefadhaishwa na jambo hili, ha—hatimaye alikuwa na. . .Alikuwa na mvulana aliyelemaa kwa polio, mguu wake umekunjamana chini yake.

61 Nikaondoka pale, huko Houston, Texas, ambako picha mliyo nayo ya Malaika wa Bwana ilipigwa. Na ule mjadala kule chini pamoja na mhudumu huyu wa Kibaptisti ambaye alichukua upande huo mwingine, kwamba Kristo hakuwa Mponyaji sasa. Ndipo Bwana akaja mbele ya watu elfu thelathini usiku huo, na kuiweka, alipigwa picha Yake, ile Nuru inayotoa utambuzi, ambayo ilionyesha kwamba ilikuwa ni kweli.

62 Naye George J. Lacy, mkubwa wa FBI, wa alama za vidole na nyaraka akaichukua, kutoka California, akaja kwenye jengo la Shell kule ndani, na kuichunguza hiyo picha, na kusema, "Bw. Branham, nimekuwa mkosoaji wako, nami nilisema ilikuwa ni saikolojia, bali," kasema, "jicho la mitambo la kamera hii halitapiga picha saikolojia. Nuru hiyo ilipiga lenzi." Na kwa hiyo ninyi mnayo hiyo picha sasa. Na moja ya hizo iko Washington, DC, katika Ukumbi wa Sanaa za kidini, ikiwa na muhtasari chini yake, "Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichopata kupigwa picha

katika historia ya ulimwengu." Na sasa, basi, kama ukiwahi kupitia kule, ingia, ukaione.

63 Sasa angalieni. Ndipo Bw. Wood akamleta mvulana wake mahali, kwenye huu, ambapo tulikuwa mahali pengine. Ndipo Roho Mtakatifu akaita na kusema, "Yupo mvulana hapa nyuma jengoni, jina lake David Wood. Baba yake ni mkandarasi. Shahidi wa Yehova." Sijawahi kuwaona maishani mwangu. Waliishi katika nchi nyingine, huko Kentucky. Na kwa hiyo Yeye akasema, "BWANA ASEMA HIVI, mvulana huyo ameponywa." Ndipo mara mvulana huyo kilema akasimama kwa miguu yake, mzima tu kama mtu mwingine yeyote. Yeye ni jirani yangu sasa. Nilimwoza, yapata miaka mitatu iliyopita kwa msichana mzuri Mkristo, nao wana watoto wawili wazuri. Watu wengi hapa wanajua hilo.

64 Mimi na Bw. Wood, tulipokuja nyumbani, tuliendesha motokaa kuteremka kwenye milima ya Kentucky, katika nchi ndogo ambako nilikuwa kwenye uwanja wa kambi wa Methodisti kule chini, mahali paitwapo Acton, A-c-t-o-n, du—duka moja tu la vyakula, kituo cha petroli, na uwanja wa kambi. Napo panaitwa Acton, Kentucky. Ma—mahali hapo padogo pana ofisi ya posta, yake, iko kwenye duka hili. Nilikuwa na mkutano pale. Napo palionekana kwangu kama eneo zuri la kuwindia kuchakulo, kwa hiyo nilitaka kurudi huko.

65 Yapata miaka miwili kutoka pale, tulirudi tena, kurudi na kuenda kuwinda kuchakulo.

66 Basi—basi, bila shaka, ninyi watu wa Arizona hapa, nadhani. . . Ni wangapi wanaojua kuchakulo wa kijivu wa Kentucky ni nini? Ni wangapi waliopata kuwaona kuchakulo wa kijivu? Loo, vema, kwani mnatoka sehemu gani ya Kentucky? Kwa hiyo basi ninajisikia nyumbani kweli. Kwa hiyo hakuna kitu bora zaidi cha kula duniani. Kama wanacho, sijawahi kukipata.

67 Kwa hiyo tukashuka kwenda kwenye likizo ya majuma mawili, kuwinda, na kulikuwa kukavu kwelikweli. Na hao jamaa wadogo, loo, jamani, jinsi wanavyoweza kuambaa! Nasi tulikuwa tukipiga risasi kwa bunduki za .22, nako kukawa kukavu sana tusingeweza kuwinda. Basi Bw. Wood akasema, "Ndugu Branham, na—najua mahali palipo na m—mtu ambaye ana yapata ekari mia tano ama mia sita, naye ana milima na mabonde kule chini, ambako maji yanatiririka kupitia kwenye kijito." Kasema, "Itakuwa na unyevu. Tungeweza kutembea chini ya hivyo vijito, tusingewashtusha." Lakini kasema, "Yeye ni kafiri."

Nikasema, "Vema, hebu twende tukamjaribu."

68 Kwa hiyo tukavuka nchi na kupitia misituni, na juu ya vilima, kitu kama mibururo midogo ya nguruwe mwitu, mpaka tukaifikia nyumba moja, na wazee wawili wenye kofia zilizoinama chini wameketi chini ya mti. Naye akasema, "Yule

ndiye upande ule mwingine.” Kasema, “Yeye ni jamaa mgumu.” Na kwa hiyo tukasimama.

69 Nami nikasema, “Labda afadhali uende, kama unamfahamu. Afadhali niketi kwenye gari.”

Akasema, “Sawa.”

70 Kwa hiyo akashuka na kutembea huku na huku. Akasema, “Mu hali gani?” Kisha kasema, “Jina langu ni Wood.” Akasema, “Jina langu ni Banks Wood.” Akasema, “Sijui tu kama ingewezekana kama tungeweza kuwinda hapa kidogo.” Kasema, “Tumekuwa tukiwinda huku kwenye kijito kingine.” Akasema, “Kumekauka kule; hatuwezi kuwinda.”

71 Akasema, “Wewe ni mvulana wa Jim Wood?” Sasa, baba yake alikuwa mfasiri katika Mashahidi wa Yehova. Yeye ni mmoja wa wafasiri. Kasema, “Mtu mwaminifu, mzuri sana!”

Akasema, “Mimi ni mwanawe.”

72 Akasema, “Vema, Jim Wood ni mmoja wa watu waaminifu kuliko wote niliopata kukutana nao.” Kasema, “Chukua tu chaguo lako, winda popote utakapo.”

73 Kasema, “Asante, bwana.” Kasema, “Nilikuja na mchungaji wangu. Nadhani ni sawa kwake kwenda.”

74 Ndipo akasema, “Humaanishi umeshuka sana inakubidi kumbeba mhubiri kokote uendako?” Naye akasema . . .

75 Nikawazia afadhali nitoke, kwa hiyo nikatoka kwenye gari na kutembea hapo. Nikasema, “U hali gani?”

76 Akasema, “U hali gani?” Naye akasema, “Wajua, nadhani kwa namna fulani mimi ni jamaa mgumu dhidi yenu enyi jamaa.”

77 Nikasema, “Vema, kila mtu na wazo lake.” Nilitaka kuwinda. Na kwa hiyo akasema basi . . . Kasema, “Nadhani unaweza, kila jamaa na wazo lake mwenyewe.”

78 Naye akasema, “Naam.” Akasema, “Sina neno dhidi yenu ila jambo moja tu.” Akasema, “Mnabwekea kwenye mti mwingine.”

79 Ni wangapi wanaojua maana ya hilo? Huyo ni mbwa mwongo, mnaona, akibweka, mtini, “kuuni yuko *hapa*,” wakati amwekwisha ondoka. Hamna kuuni huko juu. Mnaona?

Akasema, “Mnabwekea kwenye mti mwingine.”

Nikasema, “Vema, hayo ni maoni yako.”

80 Naye mama yangu daima aliniambia, alisema, “Mpe tu ng’ombe kamba ya kutosha, atajinyonga mwenyewe.” Kwa hiyo nikawazia nitampa kamba ndefu kutosha, kwa hiyo ni—nikamwacha aendelee na kuzungumza.

81 Akasema, “Vema,” akasema, “Nimekuwa kwenye nchi hii hapa . . . Lile dohani la kale kule juu ndiko nyumba ya kwanza iliungulia, yapata miaka sitini iliyopita. Baba yangu alipajenga mahali hapa. Nimeishi hapa, nikatembea sehemu hizi sasa.”

Kasema, "Nina umri wa miaka sabini na sita. Na sijapata kumwona Mungu yeyote, wala Malaika, wala chochote kingine." Kasema, "Hivyo basi," kasema, "Mimi . . . Hamna yeyote."

Nikasema, "Vema, hakika, hayo yangali ni maoni yako," nikasema.

82 Akasema, "Vema, nafikiri tu ninyi jamaa mnazunguka-zunguka mkitafuta maisha rahisi."

Nikawaza, "Loo, jamani, laiti ungalijua ni kitu gani! Ati rahisi?"

Naye akasema, "Nafikiri ninyi nyote mnapata tu riziki rahisi."

83 Nikasema, "Naam, bwana." Nikasema, "Naam. Vema," nikasema, "hata hivyo, hayo ni maoni tu."

84 Naye akasema, "Vema," akasema, "hivyo ndivyo ninavyoamini kuhusu jambo hilo." Akasema, "Mnabwekea tu kwenye mti mwingine." Kisha kasema . . .

Nikasema, "Uliwahi kuwa kanisani?"

85 Akasema, "La." Akasema, "Siamini katika kuhudhuria." Akasema, "Kulikuwako na jamaa mmoja, wakati mmoja, aliyekuja hapa yapata miaka miwili iliyopita kutoka Indiana, alikuwa na mahali fulani hapa. Walikuwa na mkutano kwenye uwanja wa kambi wa Methodisti." Kasema, "Ninasahau jina la jamaa huyo." Kisha kasema, "Kama nikiwahi kukutana naye, nataka kuzungumza naye."

Nikasema, "Naam?"

86 Ndipo Ndugu Wood akaanza kusema . . . Nami . . . Ng'ombe alikuwa mwishoni mwa kamba, kwa hiyo hataki kulizungumzia Hilo. Nikasema . . . Nikisimama pale, masharubu usoni mwangu, karibu urefu *huo*, nimelowa damu tu kila mahali, wala sikuwa nimeoga kwa majuma mawili, na kwa hiyo nyinyi mwajua.

Nikasema, "Naam, bwana." Nikasema, "Vipi kuhusu hilo?"

87 Akasema, "Vema, tuna maskini bikizee anayeishi hapa juu ya kigongo, jina lake *nanii*." Kisha kasema, "Alikuwa akifa kwa kansa." Kasema, "Yeye, tulikuwa tumempeleka huko Louisville, kwa mtaalamu wa kansa, nao wakajaribu kumfanyia upasuaji. Ilikuwa tumboni." Tena kasema, "Alikuwa ameugua sana, kupitia tumboni mwake na mfumo wa matumbo, wasingeweza kumwosha hata kwa enema. Basi wakamleta tu nyumbani akafe." Kisha kasema, "Alidhoofika sana hata wasingeweza kumweka kwenye chombo cha msalani cha kitandani tena; iliwabidi tu kutumia shuka la kuvuta." Kasema, "Mimi na mke wangu tungepanda kule, mara mbili kwa siku, na kumbadilishia malazi." Kisha kasema, "Alikuwa yuafa."

88 Ndipo kasema, "Mhubiri huyu alikuwa huku Acton." Kisha kasema, "Alikuwa huko kwa siku mbili usiku." Naye kasema,

"Dada yake anaishi hapa chini, kijito kingine, yapata maili thelathini chini. Alienda kule usiku huo. Na akasema, 'Mtu huyo kamwe hakupata kuwa nchini hapo awali.' Naye kasema, 'Alikuwa amesimama jukwaani, akaangalia huko kwenye kadiri ya watu elfu moja mia tano. Naye akasema, "Ma—mama mmoja pale, jina lake *fulani-wa-fulani*, ulipoondoka nyumbani usiku wa leo uliweka leso ndogo nyeupe mfukoni mwako, uliyoitoa kwenye kabati la marmar juu. Nayo imepambwa kidogo kwa samawati pembeni. Una dada jina lake *Fulani-wa-fulani*, anayekufa kwa kansa. Nenda, chukua leso hiyo ukaiweke juu ya dada huyo. Kwa kuwa, BWANA ASEMA HIVI, yeye ataishi."'"

89 Kisha kasema, "Yapata saa tano usiku, nilidhani walikuwa na Jeshi la Wokovu kule juu ya kilima, kelele tupu." Ndipo kasema, "Mimi . . . Nikaamka." Kasema, "Nikamwambia mke wangu, 'Vema, alikufa. Na kwa hiyo kesho asubuhi nitachukua gari langu la mkokoteni nimtoe huko.'" Ndivyo tu ungaliweza kufika mahali alipoishi. Ingekubidi kumtoa, umfikishe mahali ambapo ungeweza kumfikisha kwenye motokaa, kwa mkokoteni. "Kasema, 'Nitangojea tu mpaka asubuhi.' Kisha kasema, 'Tutaenda tumchukue, na kumtoa huko.'"

90 Kasema, "Kesho yake asubuhi, mimi na mke wangu tukaamka mapema, tupate kwenda kule juu. Basi tulipata nini tulipoingia, lakini yeye alikuwa akila sambusa za matofaa yaliyokaangwa mezani, pamoja na mume wake." Ndipo kasema, "Yeye yuko huko juu sasa. Hafanyi tu kazi yake mwenyewe, bali anafanya kazi ya jirani yake."

Nikawazia, "Aa-loo, hii hapa!"

Nami nikasema, "Sasa, huamini hilo."

91 Akasema, "Vema, kama huliamini, wewe panda uende ukajionee mwenyewe." Ananihubiria sasa.

92 "Mbona," nikasema, "katika siku ambayo tuna sayansi ya kisasa, na madaktari, na wazuri jinsi tulivyo nao, nawe unataka kuniambia kwamba ninii . . . "

93 "Vema," kasema, "kama huamini, wewe panda uende kule ukamwulize." Kasema, "Ndiye yule kule." Kasema, "Hiyo si ni kweli, John?"

94 Akasema, "Hiyo ni kweli." Huyo mzee mwingine alikuwa ni mwaminio. Akasema, "Hiyo ni kweli. Yuko moja kwa moja kule juu sasa. Unaweza kwenda ukamwulize." Sasa, yeye akinihubiria sasa, mnaona. Kwa hiyo, vema, hiyo ni sawa.

Kwa hiyo nikasema, "Vema, ungesema ni nini kilichotukia?"

95 Kasema, "Jinsi ninavyotaka kumwuliza mtu huyo, yeye alijuaje ya kwamba huyo alikuwa ni mwanamke huyo kule juu? Hakuwahi kuwa nchini hapo kabla. Alikuwa yuafa kwa kansa.

Alijuaje alikuwa akifa kwa kansa? Alijuaje jina lake? Na alijuaje huyo alikuwa ni dada yake? Tena alijuaje ya kwamba atapata afya wakati leso hiyo ilipowekwa juu yake?" Kasema, "Ninataka kuzungumza naye nitakapomwona."

Nikasema, "Loo, natumaini utafanya hivyo."

96 Kwa hiyo, nikageuka. Nayo ilikuwa karibu—karibu katikati ya Agosti, na ni joto sana na majani yalikuwa yanaanza kupukutika kutoka mitini. Naye alikuwa na mtofaa mzuri pale, na—na matofaa yametapakaa ardhini. Basi nikasema, "Ungejali kama nikiokota moja ya hayo matofaa?"

97 Akasema, "Manyigu wanayala." Ni wangapi wanaojua nyigu ni nini? Kwa hiyo, kasema, "Wanayala. Afadhali nawe uyale."

98 Kwa hiyo nikaokota moja nikalisugua kwenye hizi suruali chafu, mwajua, kisha nikaliuma. Nikasema, "Hilo ni tofaa tamu."

Kasema, "Loo, naam. Niliupanda mti huo pale, miaka arobaini iliyopita."

Nikasema, "A-ha."

"Huo, naam, bwana, niliupanda."

Nikasema, "Unazaa namna hiyo, kila mwaka?"

99 "Naam. Sisi hakika. . .Tunatia makoponi vikapu kadhaa kutoka kwake, kila mwaka. Tunakausha mengine juu ya kile kibanda."

Nikasema, "Naam, bwana." Nikasema, "Hilo ni zuri sana."

100 Nikasema, "Sasa, jambo la kigeni." Nikasema, "Unaona hata hatujakuwa na jalidi bado. Hatujakuwa na kipindi cha baridi wala chochote kile, na hata hivyo majani yote yanapukutika kwenye mti ule." Nikasema, "Nashangaa ni kwa nini hivyo?"

Akasema, "Vema, uhai uliliacha ja—jani."

Nikasema, "Ati uhai uliliacha jani?"

Akasema, "Naam."

Nikasema, "Uhai huo ulienda wapi?"

Akasema, "Chini kwenye mzizi wa mti."

"Loo." Nikasema. "Ulienda huko chini kwa kusudi gani?"

101 Naye akasema, "Vema, kukwepa kipindi cha baridi kali." Kasema, "Unaona, inafikia karibu ishirini chini ya sufuri hapa." Kasema, "Kama—kama uhai huo ungekuwa huko juu mtini, uhai huo ungekufa. Hauna budi kushuka kwenda kwenye mzizi."

102 Nikasema, "Loo, ku—kumbe. A-ha." Nami nikasema, "Ninataka kukuuliza swali." Nikasema, "Unajua mti huo hauna akili yoyote, kwa sababu ni mti tu, sehemu ya uhai wa mimea." Nikasema, "Ni akili ya aina gani inayouambia, kabla ya jalidi kuanguka, 'Ondoka humo, upesi sana. Shuka upesi mzizini

ukajifiche. Usipojificha, utakufa.' Ni akili gani inayofanya hivyo?"

"Vema," akasema, "hayo ni maumbile tu."

103 Nikasema, "Vema, nitakwambia. Hebu chukua ndoo ya maji ukaiweke kwenye nguzo huko nje, ifikapo Agosti, hebu nione maji hayo yote yakitiririka chini ya nguzo hiyo, kisha yarudi tena kwenye msimu wa kuchipua."

Kasema, "Sikuwa nimewazia hilo."

104 Nami nikasema, "Liwazie hilo wakati nikienda kuwinda kuchakulo. Halafu basi, nitakaporudi, kama utaniambia ni Akili gani inayouambia utomvu huo katika mti huo, uhai huo, 'Shuka uende mizizini ukajifiche, mpaka kwenye msimu wa kuchipua, kisha urudi tena.' Utakapojua ni Akili gani inayoamrisha uhai huo kupanda na kushuka, kupitia kwenye mti huo, kwenye misimu, nitakwambia ni Akili gani iliyoniambia mimi mwanamke huyo alikuwa anaenda kupona."

Kasema, "Ati iliyokwambia wewe?"

Nikasema, "Naam, bwana." Nikasema . . .

Akasema, "Wewe siye yule mhubiri?"

Nikasema, "Mimi ni Ndugu Branham."

Akasema, "Unaweza kuthibitisha hilo?"

Nikasema, "Hakika." Nikasema, "Nadhani sionekani kama ndiye."

105 Kasema, "La, napenda hilo." Akasema, kasema, "Unaonekana mwanadamu."

106 Nami nikasema, "Vema . . ." Nikasema, "Vema . . ." Nikasema, kwa hilo, "Vema," nikasema, "sawa, bwana."

Naye akasema, "Hivi wewe ndiwe yule mhudumu?"

107 Nikasema, "Naam, bwana. Mungu yeye yule anayeweza kunena na mti, anaweza kunena na mtu." Basi hapo nikamwongoza mzee huyo kwa Kristo.

108 Mwaka mmoja baadaye, nikarudi. Naye alikuwa ameenda kukutana na Bwana. Ndipo mke wake akaniambia, kasema, "Ndugu Branham, alikufa katika ushindi, akimsifu Mungu."

109 Ilikuwa ni kitu gani? Alimwona Mungu akinena katika ulimwengu Wake. Kati ya mambo yote aliyokuwa ameona, na hata hivyo asili yenyewe ya mti ilimtangazia ya kwamba kulikuwako na Mungu. Mnaona? Naye alilipata hilo, na akampata Yesu Kristo kama Mwokozi wake.

110 Loo, jinsi unavyoweza kumwona katika kuchomoza kwa jua, umwone katika kutua kwa jua. Kila unapoangalia, unaweza kumwona Mungu. Kama nilivyosema, hivi majuzi usiku, "Akiwa ndani yako, unaweza ukamwona *huko* nje."

111 Huko Colorado, kwa kawaida mimi huenda huko kuwinda. Basi msimu mmoja wa majani kupukutika. . .Mimi na jamaa mwingine huwinda huko juu, halafu tunatengana. Tulikuwa tukiwinda kulungu, huko juu kabisa, mpaka theluji ikaja na kuwashusha kulungu chini. Kwa kweli hao wako huko kwenye maeneo ya misitu, kwa sababu ni wanyama mwitu. Na kwa hiyo tulikuwa tumechukua farasi wa mizigo, kila mmoja wetu, na farasi wa matandiko, tukapanda juu sana. Na—naye Bw. Jeverez, mwenye ranchi hiyo, alikuwa amerudi kwa mkondo mmoja wa kijito, yapata maili ishirini, nami nikapitia njia hii nyingine.

112 Na katika msimu wa majani kupukutika mwakani, hivyo, wataninii. . .Mwajua, jua litawaka kwa muda kidogo, na mvua muda kidogo; barafu muda kidogo, mvua tena, kisha jua linachomoza. Mnajua jinsi ilivyo.

113 Ndipo tufani ikaja kupitia mlimani. Nilikuwa karibu na mpaka wa msitu. Nami nilikuwa nimemfunga farasi wangu wa matandiko, huko chini kabisa, maili kumi, kumi na mbili chini yangu, nami nilikuwa nikiendelea kuwinda, kukavu kabisa, ndipo tufani ikatokea. Basi nikaingia nyuma ya kichaka, karibu na palipoangushwa, na mahali upepo ulikuwa umeangusha miti, baadhi ya hemloki. Na kwa hiyo nilikuwa nimesimama nyuma ya miti hii mpaka u—upepo ukapita. Nayo tufani ikawa baridi. Nikasimama pale, karibu saa moja na nusu, nadhani, na nusura nigande, na huku upepo unavuma. Ndipo basi, baada ya kitambo kidogo, ukaachilia. Nami kidogo nikatikisa kichwa, na kuingiwa na usingizi kidogo.

114 Kwa hiyo nikaangalia juu, na nilipoangalia, nilikuwa nimesimama, nikitazama kote. Ndipo nikaona jua likijitokeza, wakati likitua. Na huko juu kabisa, ambapo mvua ilikuwa imevumishia, na kuififikia miti isiyokauka, na ilikuwa imeigandishia barafu juu yake. Nalo jua lilikuwa likiakisi dhidi ya hiyo barafu, nayo ikasababisha upinde wa mvua. Loo, jamani! Ningeweza kumwona Mungu huko. Huyo hapo Mungu, papo hapo, katika upinde wa mvua ya agano. Nikawaza, "Huyo hapo Mungu kule juu, juu ya mlima."

115 Halafu, baada ya kitambo kidogo, nikamsikia kulungu mkubwa wa kiume. Alikuwa amepotea kwenye tufani hiyo. Akipigia kundi hilo baragumu. Ni—ni—ningeweza kumsikia Mungu katika hiyo. Maskini mzee mbwa mwitu akaanza kuita mlimani, mwenziwe akimjibu, huko chini kabisa. Yupo Mungu katika hilo. Daima niliamini Yeye aliishi huko juu. Alikuwa Yule pale kwenye kutua kwa jua. Alikuwa Yule pale kwenye upinde wa mvua. Alikuwa Yule pale kwenye wito wa kulungu. Yule pale kwenye wito wa mbwa mwitu. Yeye yuko katika maumbile, kotekote, kila mahali.

116 Na la kunishangaza, upande wa pili tu kutoka kwangu, juu ya kisiki, aliketi maskini kuchakulo wa misonobari. Yeye

ni kama tu bundi wa Muairishi, "kelele tupu na manyoya, na hakuna bundi," mwajua. Na ni jamaa mdogo tu, ameketi huku amejikunyata, bali yeye ndiye polisi mwenye koti la samawati wa msituni. Anapopiga makelele, wanyama wote wa mwitu watatimua mbio. Na alikuwa ndiye huyu hapa, ameketi pale, akinipayukia, kana kwamba alikuwa anaenda kunirarua vipandevipande. Naye hakuwa mkubwa *hivyo*. Lakini alikuwa tu akirukaruka juu chini. Nami nikawaza, "Usisisimkwe sana, jamaa mdogo." Na kile kilichokuwa kimemsisimua . . .

117 Ni—nilisisimkwa kidogo, mimi mwenyewe, nilipoanza kuona mambo hayo yote. "Mungu," nikasema, "loo, ni mahali pazuri jinsi gani pa kuwa!" Nilijisikia kama Petro alivyojisikia, juu ya Mlima wa Kugeuka Sura, "'Hebu tujenge maskani tatu na tukae hapa.'" Nami ni—nikajaa sana utukufu wa Mungu nafsini mwangu, ni—nikaegesha bunduki yangu kwenye mti. Nami nilikuwa nikilipuka, nadhani. Nikakimbia kote, kuuzunguka mti, nikipiga makelele, "Mungu asifiwe! Mungu asifiwe!"

118 Ilibidi niachilie kitu fulani. Nacho hakikuninii . . . Kilango pekee cha kuzibulia nilichokuwa nacho, nadhani. Kwa hiyo nikaninii tu . . . Sijui kama mliwahi kujisikia vizuri hivyo au la. Bali mnaweza kufanya hivyo, maana nina ujuzi wake. Ninajua ni kweli, wakati unapoweza kuangalia huko nje na kumwona Mungu kote karibu nawe.

119 Hupati harufu ya sigara yoyote kule juu, wala hapana pombe na takataka huko, wala wanawake waliovalia nusu. Wako—wako—wako kule chini kwenye malundo ya takataka ya ibilisi.

120 Bali hii ni kule juu anakoishi Mungu. Na kwa hiyo basi, kule juu, nikikimbia kote, kotekote, nikisema, "Asante, Bwana! Nimeuona huo upinde wa mvua." Nikawaza, "Kuonekana kwake . . . "

121 Katika mlango wa kwanza wa Ufunuo, Yohana alimwona kama upinde wa mvua, kama Alfa na Omega, loo, Mwanzo na Mwisho. Akiwa na agano, kwamba asingeuangamiza ulimwengu tena. Halafu basi tumepata, katika *hili*, Agano Jipya ni agano la Damu Yake.

122 Na jinsi nilivyoanza, kupata, kupiga makelele. Sikuwa nikijifanya mnafiki. Nilijisikia vizuri, nami nilitaka kujiachilia mwenyewe. Nami nilikuwa nikipiga makelele, "Mungu asifiwe!" na kuzunguka, kuzunguka mti. Nadhani walifikiri walikuwa na mwendawazimu mwituni, kama mtu angalikuja huko. Bali sikujali ni nani aliyekuwa huko. Nilikuwa nikijisikia vizuri, nami nilitaka kufurahi katika Bwana.

123 Basi nafikiri nilimsisimua maskini kuchakulo huyo. Na, yeye, nadhani hajapata kuona kitu kama hicho. Sio kuchakulo tu, bali watu wengine wengi hawajapata kuona kitu kama hicho, au hata binadamu. Nami huyu hapa, nikizunguka. Nadhani nilionekana tamasha la kuchekesha, bali nilikuwa nikijisikia

vema. Halafu basi yeye alikuwa ameketi pale, amejikunyata kabisa, na akinipayukia-payukia. Maskini macho yake karibu yametokeza shavuni mwake.

124 Nikasema, "Usisisimkwe. Nilikuwa tu nikimwabudu Muumba wetu. Keti chini. Fanya vivyo hivyo. Utajisikia vizuri zaidi." Ndipo maskini jamaa huyo akaketi chini. Nikawaza, "Hivi huoni? Angalieni. Hii hapa. Inua mikono yako ukamsifu Bwana." Nikasema . . .

125 Ikatokea kwamba niliona. Yeye hakuwa akiniangalia mimi. Alikuwa amekiinamisha kichwa chake, akiangalia *hivyo*. Nikawaza, "Vema, kwani jamaa huyu mdogo anaangalia nini?" Nayo tufani ilikuwa imevuma na kumlazimisha tai mkubwa kushuka, kwenye mvumo huu. Na hilo ndilo lililomsisimua, yule tai akitambaa huku, kwenye kichaka hicho pale.

126 Kwa hiyo nikawaza, "Sasa, Bwana, nimekuona kwenye upinde wa mvua. Nimekuona katika kutua kwa jua. Ninakusikia katika wito wa wanyama. Na sasa, ningewezaje kamwe kukuona Wewe katika huyo tai? Wewe uko katika yule tai? Basi kwa nini ukanizuia kukusifu Wewe?" Mnaona, Mungu hufanya kila kitu sawa. Yeye alijua ningesimulia hii siku moja. Naye alikuwa ni Yule pale. Tai huyu mkubwa akaruka juu kwenye ta—tawi, kisha akaniangalia. Nami nikawaza, "Jamani, ananivutia. Haogopi."

127 Ninavutiwa na kitu chochote kisicho na woga. Mungu hawezi kumtumia mwoga. Kama wewe ni mwoga kupindukia huwezi kushuhudia mbele ya bosi wako, mbele ya mtu mwingine yeyote, na unamwonea Yesu Kristo aibu, Yeye hawezi kukutumia, kama unaionea aibu Injili ya Yesu Kristo. Nafikiri kama Paulo alivyosema, "Siionei aibu Injili ya Yesu Kristo, kwa kuwa ni nguvu za Mungu ziletazo wokovu kwa kila aaminiye."

128 Watu wengine wanaweza kupiga makelele, kanisani; bali wanapotoka nje, wanaishiwa na pumzi. Sasa, dini ya aina hiyo si nzuri. Hiyo ni ya maonyesho tu. Inapaswa kuishiwa.

129 Na kisha nikamwona tai huyu mkubwa. Hakuogopa. Nikawaza, "Vema, unajua nini? Hivi huniogopi?" Macho hayo makubwa ya kijivu yakiniangalia, Nikawaza, "Kwa nini huogopi?" Nikasema, "Ningeweza kuichukua bunduki yangu hapa na kukupiga risasi." Nikasema, "Hivi huniogopi?" Naye akaninii tu . . . Hakuwa akiniona. Alikuwa akimwangalia yule kuchakulo. Angeniangalia mimi, na kisha akamwangalia huyo kuchakulo. Nikawaza, "Ninachoshwa na kelele hiyo, pia. Nawe je?" Na kwa hiyo akaendelea tu kuangalia, huku na huku.

130 Basi baada ya kitambo kidogo, nikawaza, "Ni kitu gani kinachomfanya awe na ha—hakika sana?" Nikaona aliendelea kuyahisi mabawa yake, mwajua, kuyatimua manyoya yake katika mabawa yake. A-ha. Mnaona, hilo hapo. Mnaona, alikuwa na kipawa alichopewa na Mungu, hayo mabawa. Naye alijua, kabla sijaweza kuuweka mkono wangu juu ya

ile bunduki, angeweza kuwa kwenye msitu ule. Mnaona? Na yeye hakutishika, mradi tu angeweza kuhisi ngu—nguvu ambazo Mungu alikuwa amempa, kwenda mahali pa salama.

131 Loo, laiti Mkristo angaliweza tu kufanya hivyo! Kama tai aliweza kuweka matumaini kiasi hicho katika jozi ya mabawa yamwondoe hatarini hadi kwenye usalama, ni zaidi sana jinsi gani inavyompasa mwanamume ama mwanamke aliye katika Uwepo wa Yesu Kristo, ambapo Yeye anajitambulisha Mwenyewe, kuogopa chochote? Hmm? Kama unaweza kujua na kuona, kuona Biblia ikisema itakuwa *hivi*, na hapa ipo hapa, Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, akitembea miongoni mwetu, akifanya jambo lile lile Yeye alilofanya daima, na aliahidi Yeye angelifanya kabla tu ya wakati wa mwisho, tungewezaje kuogopa? Hakuna kitu kitakachowadhuru. Kinawezaje kuwadhuru? Yeye alishinda, na kushinda kila kitu: mauti, kuzimu, kaburi, maradhi, kila kitu kingine, dhambi. Yeye ni . . . Mimi ni mkamilifu ndani Yake. Sio mimi mwenyewe; sina chochote. Bali ndani Yake mimi ni salama.

Nilimwona akiendelea kufanya hivi.

132 Mtu fulani aliniambia wakati mmoja, kasema, "Ndugu Branham, hivi huogopi utamleta mtu jukwaani wakati mmoja, na ufanye kosa?" Sivyo mradi tu ninaweza kumhisi Yeye akiwa karibu, halitakuwa kosa lolote. Hiyo ni kweli. Daima itakuwako.

133 Mwajua, aliketi pale mpaka akachoka, akimsikiliza maskini kuchakulo huyo mdogo pale, akipayuka, payuka, payuka. Kwa hiyo akafanya tu mruko mmoja mkubwa. Akapigapiga mabawa yake kama mara mbili, nami nikaona kamwe hakuyapigapiga mabawa yake tena. Alijua tu jinsi ya kuweka mabawa yake. Ndipo upepo ulipoingia, yeye alichukuliwa tu na upepo. Nao upepo ungeingia tena; yeye akachukuliwa tu juu na upepo huo tena. Naye akachuliwa tu na wimbi baada ya wimbi. Nami nikasimama na kumwangalia mpaka akawa ni doa dogo tu angani. Akaenda mbele zaidi, zaidi, zaidi, zaidi.

134 Nikasimama pale, nikaanza kupangusa machozi usoni mwangu. Nikasema, "Jambo ndilo hilo, Mungu. Ninaona ni kwa nini Wewe ulimtuma huyo tai hapa." Mnaona?

135 Sio ati uruke na uwe Mmethodisti juma hili, kisha uruke huko na uwe Mbaptisti juma lijalo, na kupigapiga, kupigapiga kwa moja, kisha kupigapiga, kupigapiga, kwa lingine. Bali ni kujua jinsi ya kuweka mabawa yako ya imani katika nguvu za Roho Mtakatifu. Na kama inavyokuja kama ma—mafuriko yavumayo, bebwa juu ya mawimbi yake. Ondokea maskini mpayuko, mpayuko huu wenye mawazo ya dunia, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hakuna uponyaji wa Kiungu," kupayuka, kupayuka hapa; na kupayuka, kupayuka pale. Weka tu mabawa yako katika nguvu za Roho Mtakatifu, na umwache Yeye akubebe juu

ya kelele hizi zote za mipayuko, mipayuko, kwamba, "Hakuna kitu kama hicho."

136 Huyo tai alijua kile alichokuwa akifanya. Angeweza kutumainia. Mnaona? Mungu yuko katika ulimwengu Wake. Hivi hamwamini hilo? Mnamwona Mungu katika ulimwengu Wake? Mnaweza kumwona katika ndege. Mnaweza kumwona katika maua. Mna...Loo! Tungeweza kutumia usiku wote juu ya hilo. Lakini mnaamini ya kwamba Mungu yuko katika ulimwengu Wake?

137 Vema. Sasa tutaona kama Mungu yuko katika Neno Lake. Sasa tutamwangalia Mungu katika Neno Lake. Si kwamba tu Yeye yuko katika Neno, bali Yeye ni Neno. Hiyo ni kweli. Biblia ilisema katika Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu." Mungu na Neno Lake ni sawa.

138 Neno, Yesu alisema, ni Mbegu ambayo mpanzi alipanda. Na mbegu yoyote iliyorutubishwa kwenye udongo mzuri itazaa kwa jinsi yake.

139 Na sasa ninatambua ya kwamba haya yanarekodiwa. Na kanda hizi, tuna huduma ya kanda, kote ulimwenguni. Na watu wengi, hapa tu usiku wa leo, ambapo yapata watu elfu moja wanasikiliza. Kabla kanda hii haijasimama, kutakuwako na watu elfu kumi mara kumi watakaoisikiliza, mnaona, kote ulimwenguni.

140 Nami ninaingia kwenye kumbukumbu, nasema hili, kuhusu Neno la Mungu kuwa ni Mbegu. Kama unaweza kuchukua msimamo mzuri wa kiakili kuhusu ahadi yoyote ya Kiungu ya Mungu, Yeye ataitimiza, kama unaweza kujiweka mwenyewe katika mahali pa kuamini ya kwamba ahadi hiyo ilikuwa kwa ajili yako.

141 Lakini ukimwacha riki fulani kuliweka mbali, kwa elimu nyingi kuliko ajuavyo akili za kutosha kujua jinsi ya kuidhibiti, anaweza kuibandika kwenye wakati fulani uliopita, ama wakati fulani ujao, haitakuwa na nguvu kwako. Kama vile Yesu alivyosema, "Mnachukua mapokeo yenu na kuzitangua amri za Mungu," mnapojaribu kumweka Mungu kuwa Mungu fulani wa kihistoria, ama mtangulizi Mungu ajaye.

142 "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Yeye ni Mungu tu sasa kadiri alivyowahi kuwa. Na laiti ungaliweza kuchukua msimamo huo, kwamba ahadi hiyo ni kwa ajili yako! Yesu alisema, katika Marko Mtakatifu 11:22, "Amin nawaambia, ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' usitie shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako. Ninasema, mwombapo, aminini kwamba mnapokea mliyoomba, mtapewa." Ni ahadi zaidi jinsi gani ingefanywa

kuliko Hiyo? Huna budi kuliamini, kwa sababu ni mbegu. Sasa, kama mimi . . .

143 Kama ukiniomba mwaloni, nami nikupe mbegu ya mwaloni, kwa uwezekano ungekuwa na mwaloni. Uko katika umbo la mbegu. Na wakati unapomtaka Mungu maishani mwako, mkubali tu kama Mwokozi wako. Kwa uwezekano, wewe ni mwana wa Mungu wa kiwango kikamilifu. Utakua ufikie kiwango cha Mungu. Kama tu vile hiyo mbegu ya mwaloni ifanyavyo, hukua ikawa mwaloni.

144 Sasa, ninyi watu hapa Arizona, hukuza machungwa. Kwanza, ni mbegu. Mbegu inaoza. "Mbegu, punje ya ngano, haina budi kuanguka ardhini," kama Yesu alivyosema kuhusu nafsi Yake. Haina budi kuoza.

145 Na jambo pekee unaloweza kufanya ni ku—kuninii . . . Njia pekee, ni kuikubali hiyo chembe ya Uzima wa Neno la Mungu, Uzima wa Mungu Mwenyewe, kisha uyaozee mawazo yako mwenyewe. Acha Mungu afanye hilo.

146 Si kazi yangu kujaribu kulielewa. Siwezi kulielewa. Ninaliamini tu. Kamwe hakuniomba nilielewe. Kamwe Yeye hakusema, "Ulilihisi Hilo?" Kamwe hakusema, "Ulilielewa?" Yeye alisema, "Uliliamini Hilo?" Hivyo ndivyo ilivyo.

147 Usijaribu kwenda kwenye seminari fulani na kushindiliwa ndani yako baadhi ya hii kasumba ya dawa ya kuhifadhi maiti, ya kanuni fulani ya imani ya kijamii. Kitu unachohitaji ni ubatizo wa Roho Mtakatifu, ngu—nguvu zilizofanyika mwili za Mungu anayeishi ndani yako, ambaye hukubali hili Neno na kulifanya Hilo liishi kama Hilo lilivyo hasa. Nikizunguka na kuzunguka ulimwengu, na mbele ya kila namna ya watu, ninajua kwamba ni kweli. Yeye ni Mungu.

148 Sasa, maskini mchungwa huo, kama uko chini ya . . . Sasa, unapoupanda, labda unapouchukua, ni chipukizi, kimelea, yapata ukubwa *huu*. Sasa, unaupanda. Sasa, hayo ndiyo yote unayopaswa kuufanyia. Haikubidi kwenda na kusema, "Sasa, sina budi kujiokotea machungwa mahali fulani, kisha niende nikayashindilie ndani yake." Machungwa tayari yamo ndani yake.

149 Jambo pekee ambalo mti huo mdogo unapaswa kufanya. Inakupasa kuweka maji mengi juu yake. Halafu basi jambo pekee huo mti unalopaswa kufanya ni kunywa. Nao unakunywa na kunywa, mpaka unakunywa kupita kipimo chake. Na wakati unapokunywa, unayasukuma matawi. Nao unakunywa zaidi, kisha unasukuma majani. Unakunywa zaidi, unasukuma maua. Unakunywa zaidi, unayasukuma machungwa. Kunywa tu na kusukuma, kunywa na kusukuma, hivyo.

150 Na huo ni wewe. Tunapopandwa pamoja katika Kristo, jambo pekee tunalopaswa kufanya ni kunywa kutoka kwa ahadi Yake, na kusukuma. Kila kitu ulicho na haja nacho kimo ndani

yako unapompokea Kristo, maana Kristo yuko ndani yako. Na inakubidi tu kunywa kutoka kwa Neno Lake, Uzima Wake, na kusukuma nje. Loo, naam. Ninamwamini Yeye kuwa ndiye Maji yanayokuja juu yetu. Yeye ni Uzima. Ninaamini Yeye ni Chemchemi ya Uzima isiyokwisha, kwamba tumepandwa tu ndani Yake na kusukuma nje.

151 Ibrahimu alimpokea Mungu katika Neno Lake, alipokuwa mzee, umri wa miaka sabini na mitano. Sara alikuwa na sitini na mitano. Alikuwa amekata hedhi kwa kadiri ya miaka ishirini. Yeye alikuwa ameishi naye tangu mke alipokuwa na umri wa yapata miaka kumi na minane. Dada yake wa kambo; akamwoa. Naye Mungu akamjia mzee huyo siku moja, na kumwambia atapata mtoto kwa Sara. Nalo Neno hilo, Neno hilo, Mungu katika Neno Lake! Wakati Mungu aliponena hilo kwa Ibrahimu, hoja zote za chochote kinyume chake zilimwondoka.

152 Hivyo ndivyo unavyofanya unapomwona Mungu katika Neno Lake. Huna budi kulipokea namna hiyo, hata hivyo. Unaona?

153 Neno lako halifi. Ningeweza kuzungumza hapa, kwa—kwa chombo cha kueneza, nayo maneno yangu yatauzunguka ulimwengu katika dakika moja. Kupitia jengo hili usiku wa leo zinakuja picha za watu. Hebu fungua televisheni yako uone kama sivyo. Maneno ya watu yanapitia hapa. Huyaoni. Hisi zako haziyatangazi, bali yapo. Wala Neno halifi.

154 Hapa si muda mrefu uliopita niliona ono la mwanamke huyu kijana akifa, ambaye walisema alijiua. Imekuwa yapata mwaka mmoja uliopita. Ninasahau . . . Alikuwa namna fulani ya msichana aliyekuwa mwanamke maarufu sana. Nami nilikuwa huko juu milimani. Nikamwona akifa. Nao wakaniambia, kasema . . . Yeye akaniambia, kasema, "Sasa, yeye . . . Unaweza kusema ni saa kumi. Ni sekunde chache tu kabla ya saa kumi." Kisha kasema, "Watasema alijiua, bali alikufa kwa mshtuko wa moyo." Jina la mwanamke huyo ni nani? Alininii tu . . . Mwanamke kijana mwenye nywele nyeupe, Marilyn Monroe. Hilo lilikuwa ndilo. Yeye, alikufa, na—na hakujiua.

155 Nilimhurumia msichana huyo. Daima alionekana kuwa ni namna ya mwanamke, mchovu, alihitaji kitu fulani. Laiti ningaliweza kumfikia mtoto huyo. Alimhitaji Kristo. Huenda alihudhuria kanisa fulani baridi, la kawaida. Lakini alihitaji kisa halisi cha wokovu, pamoja na kitu fulani moyoni mwake, kumpa hilo hakikisho. Yeye . . . Baba yake, kamwe hakumwona. Mama yake alikuwa katika hospitali ya wendawazimu. Yote yalikuwa kwenye nia ya msichana huyo. Alimhitaji Kristo. Halafu basi, katika hilo, tunajua hilo.

156 Hivi majuzi usiku, watoto wangu walikuwa wakiniambia ya kwamba kwenye televisheni walikuwa wanaenda kuwa na sinema inayoitwa "Mto wa Kutokurudi." Huko ndiko

nilikomvua yule samaki aliyevunja rekodi ya dunia, huko chini wakati mmoja pamoja na Wafanyabiashara Wakristo. Nao walitaka nione kama huo ulikuwa ndio ule mto; twende mahali palipo na televisheni na tuuone, kama huo ulikuwa ndio ule mto, na kama Don Smith, yule kiongozi, alimpeleka msichana huyu huko chini. Alikuwa ndiye huyo hapo kwenye televisheni, msichana yule yule niliyemwona, naye alikuwa amekufa kwa mwaka mmoja. Lakini pale, kila hatua aliyopiga ilikuwa pale pale, akicheza, sauti yake, hai. Sasa, huo ni katika kama kiwango cha nne. Na jambo lilo hilo litampata kila mmoja wetu kwenye Siku ya Hukumu.

157 Basi wakati Yesu Kristo aliponena Maneno haya, kamwe hayafi. Sayansi inadai, katika miaka ishirini tangu sasa wanaweza kuishika Sauti yenyewe. Wataweza kushika Sauti yenyewe ya Yesu. Ingali duniani. Maana, mnaona, ni kituo cha kutuma, wewe ndiwe. Basi hapana budi pawe na kituo cha kupokea. Na kama unaweza kuwa ndiye kipokezi, unaona, kituo cha kupokea, kulipokea Neno la Mungu, basi Hilo ni halisi kwako, na Hilo litaishi kama tu lilivyokuwa wakati huo. Amina.

158 Sasa, Ibrahimu aliichukua. Mungu alisema, “Utapata mtoto kwa Sara mkeo.”

159 Sasa, kwa akili ya kawaida, huo ni upumbavu. Ungeweza kuwazia mtu mkongwe, umri wa miaka sabini na mitano, na mkewe umri wa miaka sitini na mitano, wakishuka kuja na kusema, “Sasa, daktari, tunataka kufanya maandalizi ya hospitali”?

“Mbona,” walisema, “mzee huyo amerukwa na akili.” Mnaona?

160 Lakini watu wote ambao wanamwamini Mungu kwenye Neno Lake, kwa ulimwengu, wanahesabiwa kidogo wamerukwa na akili, kwa sababu mambo ya ulimwengu huu ni ya kimwili, kwa Mungu. Nako kuhubiriwa kwa Injili, na Mkristo, ni upumbavu kwao wanaoangamia, pia.

161 Lakini Ibrahimu aliliamini. Ninaweza kumwona Sara akishona vijiatu vidogo, mwajua, na kuandaa vipini, naye yuko tayari. Mwezi wa kwanza ukapita, na, mnaona, yeye akasema, “Mpenzi, unajisikiaje?”

“Hakuna tofauti.”

“Utukufu kwa Mungu. Tutampata, haidhuru.”

“Kwa nini?”

“Mungu alisema hivyo.”

Mwaka mmoja ukapita. “Unajisikiaje, Sara?”

“Hakuna tofauti.”

“Tutampata, kwa vyovyote vile. Haleluya!”

“Unajuaje utampata?”

"Mungu alisema hivyo." Ni Neno, Mungu aliahidi.

162 Miaka ishirini na mitano baadaye, miaka ishirini na mitano baadaye, yeye akiwa na umri wa miaka mia moja, naye mke tisini, maskini bikizee aliyevaa shali ya begani, na kijikofia cha vumbi. Fimbo, ameishika namna *hii*, naye mume ni mkongwe, huku ndevu zake zimening'inia chini. "Unajisikia tofauti yoyote, mpenzi?"

"Hata kidogo, mpenzi."

163 "Utukufu kwa Mungu! Tutampata, haidhuru. Mungu alisema hivyo." Mnaona?

164 Haya basi. Halafu ati tunajiita wenyewe uzao wa Ibrahimu? Haijalishi, mbona, itakuwa ninii kubwa sana . . . Angeweza kumsifu Mungu zaidi, miaka ishirini na mitano baadaye. Itakuwa ni mwujiza mkubwa zaidi.

165 Lakini tutamwona Yesu Kristo akijidhihirisha Mwenyewe moja kwa moja mbele zetu, na kama Yeye hatafanya jambo mara moja, "Nililikosa. Sikulipata." Ati uzao wa Ibrahimu? Mnaona?

166 Mungu katika Neno Lake! "Mbingu na nchi zitapita," kasema Yesu, "bali Maneno Yangu hayatashindwa kamwe." Mungu yuko katika ulimwengu Wake. Mnaamini hilo? Mungu yuko katika Neno Lake.

167 Wakati maskini watu waoga, mia moja na ishirini, ambao walikuwa wametembea pamoja na Yesu kwa miaka mitatu na nusu, duniani, walikuwa wamemwona Yeye akiwafufua wafu, na kutenda miujiza, na ishara, kadhalika . . . Waliogopa tishio la Wayahudi. Walipanda kwenye chumba cha juu nje ya jengo, vile vipandio vilivyoelekeza juu hekaluni, kuingia kwenye maskini chumba cha juu, chumba kidogo cha maombi upande wa nje, ambamo mishumaa midogo ya mafuta ya mizeituni ilikuwa ikiwaka, ama taa zenye utambi ndani yake. Nao wakapanda kule juu na kuifunga milango, kwa sababu waliwaogopa Wayahudi.

168 "Ndipo basi ilipotimia Siku ya Pentekoste, kukaja uvumi kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu ukienda kasi, na Huo ukaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi." Mara milango ikafunguka, madirisha yakafunguka, wakaingia mtaani, wakishuhudia chini ya nguvu, matokeo ya Roho Mtakatifu. Kwa nini? Neno la Mungu lilikuwa limedhihirishwa kwao. Mungu alitimiza Neno Lake. Hamna woga basi, Neno linapotia nanga.

169 Nitasimama hapa kwa dakika moja tu kusema jambo hili. Wakati mwanamume au mwanamke, sijali daktari anasema kiasi gani, "Unakufa kwa kansa, ukoma," ama chochote kile. Unapoweza kulipokea Neno hilo, ambalo ni Mungu, jambo fulani litatukia. Na hakuna mtu atakayekwambia vinginevyo. Unajua unalofanya. Naam, bwana.

170 Mnaamini Mungu yuko katika ulimwengu Wake? Mnaamini Mungu yuko katika Neno Lake? Bila shaka, Yeye yuko katika Neno Lake. Sasa, Mungu katika Mwana Wake.

171 Mungu katika ulimwengu Wake. Mungu katika Neno Lake. Unamwona Mungu katika ulimwengu Wake.

172 Unamwona Mungu katika Neno Lake, kwa sababu Yeye ni Neno. *Hilo* ni Mungu katika maandishi. Hilo ni Neno lililochapishwa, lakini Hilo pia liko hewani, kama mnaweza kulipokea Hilo. Loo, jamani!

173 Kama maskini mwanamke yule, aligusa upindo wa vazi Lake, akaupokea. Mnaona? Haidhuru ilikuwa ni nini, yeye alijua moyoni mwake, kama angeweza kumgusa Yeye, angeponywa.

174 Na sasa angalieni, Mungu ndani ya Mwana Wake. Loo! Yohana 14:8, Yesu alisema, "Mimi na Baba ni Mmoja. Baba anaishi ndani Yangu. Si Mimi ninayetenda hizi kazi. Ni Baba Yangu anayeishi ndani Yangu; Yeye hutenda kazi. Amin, amin nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe." Yohana Mtakatifu, mlango wa 5 na kifungu cha 19, "Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile ambalo amwona Baba analitenda." Mnaona? "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake."

175 Sasa, watu wengi huchanganyikiwa kabisa na utatu, unapoanza kuuwazia. Wengine wanaufanya watu watatu mbalimbali, na wengine wanaufanya mmoja, nao wote wawili wamekosea. Angalieni, si Miungu watatu.

176 Ni madhihirisho matatu ya Mungu yule yule. Mnaona? Ni sifa tatu. Mungu, Baba, aliyekuwa nyikani, katika umbo la Nguzo ya Moto; na halafu Mungu yuyo huyo akajidhihirisha Mwenyewe ndani ya Mwana Wake, ambaye alikuwa ni Mungu yeye yule katika Mwana Wake; na sasa Mungu yuyo huyo sasa anajidhihirisha Mwenyewe katika mimi na wewe, kama Roho Mtakatifu. Mungu yeye yule, wakati wote, si Miungu watatu; madhihirisho matatu ya Mungu yule yule, sifa tatu za Baba. Hicho ndicho alichokuwa. Yeye aliionyesha, kama Mwana. Hicho ndicho alichokuwa. Na sasa kama Roho Mtakatifu ndani ya watu Wake.

177 Mungu, akijishusha; hawezi kuguswa, kwa sababu dhambi. Halafu, Mungu Mwenyewe alifanywa kuakisiwa katika Mtu, kwa sababu mwanadamu alifanywa katika mfano wa Mungu. Naye Mungu akafanywa katika mfano wa mwanadamu, kusudi apate kuteseka, ili Yeye aweze kuondoa dhambi. Ndipo basi . . .

178 Na sasa Yeye yuko ndani yetu. "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona Mimi tena, hata hivyo Mimi nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Mungu ndani yetu. Mnaona?

Sasa, sasa inaonekana hivi, kwamba mtu yeyote angeweza kuona.

179 Mara nyingi, watu husema Yesu alikuwa ni Myahudi. Baadhi yao walisema Yeye ni nusu Mmataifa, nusu Myahudi. Hakuwa yeyote wao. Yeye alikuwa ni Mungu. Hivyo ndivyo Yeye alivyokuwa.

180 Sasa kumbukeni, mtoto anapozaliwa, uhai wowote hutoka kwenye jinsia ya kiume. Chembe ya uhai hutoka kwenye himoglobini, damu. Nayo damu ni . . . Uhai uko katika damu. Biblia ilisema hivyo. Sasa ninii . . . kama ninii—ninii—ninii . . .

181 Ni majira ya kuchipua. Na sasa ndege wote wanatengeneza viota, nao wanajaza mayai kwenye kiota. Sasa, maskini mama ndege anaweza kutoka nje hapa na kukifanya kiota chake cha kupendeza sana, na kukipamba kabisa kwa aina zote za manyoya. Naye anaweza kutaga mayai yaliyojaza kiota, na kuyalalia hayo mayai kwa uaminifu sana. Mpaka, a—angeweza kuyageuza, kila siku, vizuri kabisa. Naye angeweza kuyazunguka-zunguka, na—na kuyahifadhi yakiwa na joto, mpaka hivi kwamba hataninii . . . Atajinyima chakula hata kufa. Atakuwa dhaifu sana hata hawezi kutoka kwenye kiota, kwenda kujitafutia chakula. Anaweza kuwa mwaminifu sana kwa mayai hayo, kwa watoto wake wanaokuja! Lakini ikiwa huyo ndege wa kike hajawa katika uhusiano na ndege wa kiume, kamwe hayataanguliwa. Hana budi kuwa katika uhusiano na wa kiume.

182 Inanikumbusha juu ya makanisa leo hii. Wakati mwingine tunaweza kujenga kanisa la kupendeza kuliko yote, tuliyo nayo, na tuwe na kundi lililo bora kuliko yote la mashemasi na kila kitu kingine namna hiyo; na kusanyiko kubwa, meya wa mji, na kila mtu akilihudhuria, na kulijivunia. Bali kama hawajawa katika uhusiano na Kuzaliwa upya, pamoja na yule Mume, Kristo, una kiota kilichojaa mayai yaliyooza. Yatakaa hapo na kuoza, kila moja ya hayo.

183 Tunachohitaji leo hii ni kusafishwa kuzuri kwa kiota mtindo wa kale, kotekote kuanzia Wapresbiteri, Wabaptisti, kotekote chini, Pentekoste na wote. Huna budi kuwa katika uhusiano na Yesu Kristo, Uzima. Yeye Ndiye. Kuku anaweza kutaga yai, bali halitaanguliwa isipokuwa amekuwa na ndege wa kiume.

184 Naye Mungu Mwenyezi, Mungu Baba, alimtia uvuli bikira Mariamu, na kuumba tumboni mwake chembe ya Damu ambayo ilimzaa Mwana wa Mungu pasipo tamaa ya kujuana kimwili. Nayo hiyo Damu ilimwagwa Kalvari. Haleluya! Hiyo ndiyo Damu ninayotegemea, usiku wa leo, wakati hakuna chochote. "Hakuna chemchemi nyingine nijuayo, hakuna chochote ila Damu ya Yesu." Hivyo basi, Damu ya Mungu hutuokoa. Damu ya Mungu humleta Yesu Kristo miongoni mwetu. Damu ya Mungu humleta Roho Mtakatifu. Si Damu ya Myahudi wala ya Mmataifa; bali Damu umbaji ya Mungu Mwenyewe. Yesu,

yule Mtu, alikuwa Mwana Wake aliyemwumba Yeye Mwenyewe, kisha Mungu akafanya maskani katika maskani hiyo. Basi Mungu. . .

185 Sheria pasipo na adhabu si sheria. Kama ukisema inakiuka sheria kuvuka taa nyekundu, na hapana adhabu kwake, basi si sheria.

186 Nayo sheria ya Mungu ina adhabu. "Siku utakapokula kutoka kwake, siku hiyo utakufa." Basi mtu alipokula kutoka kwake, hakuna. . .

187 Mungu asingeweza kumtuma mtu mwingine kupachukua mahali hapo. Ingekuwa si haki tena. Kwangu kumfanya ndugu *huyu* kufa kwa ajili ya yale ndugu *huyu* amefanya, ingekuwa si haki. Ilibidi Mungu aje, Mwenyewe. Na njia pekee Yeye angaliweza kufanya hivyo, ingekuwa ni kuja katika mwili Wake Mwenyewe, ambao ulikuwa ni mwili Wake Mwenyewe muumbaji ambao Yeye aliumba, Mwenyewe, ili Yeye aweze kupatwa na mauti. Amina.

188 Hiyo hapo Injili katika nguvu. Huyo ni Mungu akidhihirishwa katika mwili, Imanueli, kuziondoa dhambi za ulimwengu. Na katika hiyo Damu tunatumaini; si katika Myahudi wala Mmataifa; bali katika Damu ya Mungu, ambayo ilikuwa ni Yesu Kristo. Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Baba Yangu anaishi ndani Yangu." Ilikuwa ni Baba Ndani Yake.

189 Mwanamke fulani alisema, "Kwani Yeye aliomba kwa nani, katika bustani ya Gethsemane," kwenye mkutano wa mtaani wakati mmoja.

190 Nikasema, "Ninataka kukuuliza jambo fulani. Ulishuhudia ulikuwa na Roho Mtakatifu. Yuko wapi? Unamwomba nani?" Yuko ndani yako, bila shaka.

191 Vema, tuna Roho kwa kipimo. Yeye alikuwa na Huyo pasipo kipimo. Sisi ni wana na binti za Mungu, kwa kipimo. Kama kuchukua maji yaliyojaa kijiko kutoka baharini, na Yeye ndiye bahari nzima, bali kemikali zile zile zilizo kwenye kijiko hicho zimo kwenye bahari yote. Ni wingi, lakini ubora ule ule. Hivyo basi, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele," Mungu yuko ndani yetu. Naam. Angalia.

Mungu katika ulimwengu Wake. Mungu katika Neno Lake. Mungu katika Mwana Wake.

192 Sasa, katika siku hii ambamo wahubiri wa injili ya kijamii, ndugu, wanajaribu kumfanya Yeye namna fulani ya nabii tu, ama—ama mwanafalsafa fulani mzuri, ama kitu kama hicho. Yeye alikuwa ama ni Mungu au mdanganyifu mkubwa kuliko wote ulimwengu uliyepata kuwa naye. Yeye alikuwa ni Mungu; si chochote pungufu, si chochote cha zaidi.

193 Mwanamke fulani alikuwa mfuasi wa dini fulani potovu isiyoamini katika kuzaliwa halisi kwa Yesu na bikira, hawalikubali. Wanaamini tu ni kutumia uwezo wa akili kutatua mambo ya kimwili. Naye huja kunisikiliza nikihubiri mara nyingi sana. Usiku mmoja alikutana nami nikitoka nje. Akasema, "Ndugu Branham, ninapenda kukusikia ukihubiri."

Nikasema, "Asante."

Akasema, "Ninapata tu kosa moja kwako."

194 Nikasema, "Vema, Bwana ashukuriwe. Natumaini Bwana anapata tu hilo, moja tu." Kisha nikasema, "Jamani! Makosa mengi kama niliyo nayo, nawe unapata tu moja la hayo?" Nikasema, "Asante, sana." Nikasema, "Naweza kuuliza kosa hilo ni lipi?"

Akasema, "Ndiyo. Unajivunia Yesu kupita kiasi."

195 Nikasema, "Hakika nitaingia, kama hilo ndilo kosa tu nililo nalo, kama ninamjivunia Yeye," nikasema.

Kasema, "Unamjivunia kupita kiasi."

Nikasema, "Una maana gani, ninamjivunia Yeye?"

Akasema, "Vema, unamfanya Mungu."

Nikasema, "Alikuwa Mungu."

196 "Loo," akasema, "Bw. Branham, umekosea, hapo." Kasema, "Yeye alikuwa ni Mtu mwema."

Nikasema, "Yeye alikuwa zaidi ya Mtu mwema."

Kasema, "Alikuwa ni nabii."

197 Nikasema, "Yeye ni zaidi ya nabii. Alikuwa ni Mungu wa manabii."

198 Naye akasema, "Loo, Bw. Branham!" Kasema, "Kama nikikuthibitishia. . .Ulisema wewe ulikuwa wa kimsingi. Basi iwapo, wewe, nikikuthibitishia, kwa Biblia yako mwenyewe, ya kwamba Yeye hakuwa Mungu, utakubali?"

Nikasema, "Kama Biblia ilisema hivyo, ninaamini Biblia."

199 Akasema, "Vema, nitakupa Maandiko yako mwenyewe." Kasema, "Yohana Mtakatifu, mlango wa 11. Biblia ilisema, kwamba, 'Wakati Yesu aliposhuka kwenda kwenye kaburi la Lazaro,' Biblia ilisema, 'Alilia.' Na Yeye asingeweza kulia na awe ni Mungu."

200 Nikasema, "Huo ndio mwisho wake?" Nikasema, "Hayo tu ndiyo uliyo nayo kusema?"

Akasema, "Ndiyo."

201 Nikasema, "Mama, hoja yako ni nyembamba kuliko mchuzi uliopikwa kwa kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa." Nikasema, "Mbona, unajua. Unajua vizuri zaidi ya hilo."

Naye akasema, "Una maana gani kwa hayo?"

202 Nikasema, “Mbona, wewe, angalia hapa. Hebu nikuonyeshe kitu fulani.” Nikasema, “Yeye alikuwa Mwanadamu, lakini unakosa kuona Yeye alikuwa ni zaidi ya Mwanadamu.” Nikasema, “Yeye alikuwa ni mwanadamu wakati alipokuwa akilia. Alikuwa mwanadamu wakati aliposimama pale, na maskini mabega yaliyoinama, kabisa, wakati, Biblia ilisema, ‘Hakuwa na uzuri hata tumtamani.’ Alikuwa ni mwanadamu amesimama pale namna hiyo, akilia. Lakini wakati alipolivuta maskini bega hilo juu, akaangalia juu kuelekea Mbinguni, akasema, ‘Lazaro, njoo huku,’ naye mtu aliyekuwa amekufa siku nne akasimama kwa miguu yake akaishi tena, huyo alikuwa ni zaidi ya Mwanadamu. Mwanadamu hawezi kufanya hivyo. Huyo alikuwa ni Mungu ndani ya Mwana Wake.”

203 Mnaamini hilo? Naam, bwana. Ninii Yake . . .

204 Mtu huyo aliyekufa, mbona, alikuwa ameharibika. Kwa maneno mengine, alikuwa ameoza. Kasema, “Ananuka.” Nafsi yake ilikuwa imeenda safari ya siku nne mahali fulani. Hatutabishana juu ya hilo, popote ilipokuwa. Lakini chochote ilichokuwa, uharibifu ulijua Bwana wake. Haleluya! Nayo nafsi ilijua Muumba wake na Mpenzi wake. Nayo nafsi iliyokuwa imeondoka kwenye mwili uliooza, siku nne, ikasimama kwa miguu yao na kuishi tena. Hebu niambie mwanadamu anayeweza kufanya hilo? Huyo alikuwa ni Mungu katika Mwana Wake, akifanya hilo.

205 Nitakubali ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwanadamu, mwenye njaa, wakati aliposhuka kutoka Yerusalemu usiku ule, akiangalia kote, juu ya mti, akijaribu kupata kitu cha kula. Alikuwa ni Mwanadamu. Hiyo ni kweli. Lakini wakati alipochukua biskuti tano na samaki wawili, na kuwalisha watu elfu tano, wakaokota vikapu kumi na viwili, huyo alikuwa ni zaidi ya Mwanadamu. Huyo alikuwa ni Mungu, Muumba, akisimama pale. Angeweza kuyageuza maji yakawa divai. Angeweza kuchukua biskuti na kuzidisha chakula, na samaki. Mungu alikuwa ndani ya Mwana Wake, kabisa. Naam.

206 Yeye alikuwa ni Mwanadamu wakati alipokuwa amelala kwenye maskini ule mtumbwi wa kale usiku ule, nao ulikuwa ukirushwa-rushwa juu chini. Amechoka sana kutokana na kuona maono, na nguvu zikimtoka, na kuhubiri Injili, kuwaponya wagonjwa, na kukosolewa na kila mtu, Yeye alirudi nyuma ya chombo hicho akalala chini. Huyo alikuwa ni Mwanadamu akilala kule nyuma, amelala usingizi. Kwenye wakati huo, pepo elfu kumi wa baharini waliapa wangemzamisha Yeye usiku huo. Alikuwa ndiye Huyo hapo, amechoka sana asingewea kusogea. Hata mawimbi yasingeweza kumwamsha. Maskini mtumbwi huo, kama kizibo cha chupa kwenye bahari yenye hasira, bado haukumwamsha. Yeye alikuwa ni Mwanadamu. Alikuwa na usingizi. Alikuwa amechoka. Alikuwa amedhoofika.

207 Bali hapo alipoamshwa, akatembea pale na kuwaangalia wanafunzi Wake, kasema, “Loo, enyi wenye imani haba,” akaweka mguu Wake demani mwa mtumbwi. Akaangalia juu, kasema, “Amani, tulia.” Nazo pepo na mawimbi yakamtii Yeye. Huyo alikuwa ni zaidi ya Mwanadamu akinena kutoka pale. Huyo alikuwa ni Mungu akinena kutoka kwa Mwana Wake. Naam, bwana. Mungu alikuwa ndani ya Mwana Wake. Ninaamini alikuwa ni Mungu. Hiyo ni kweli.

208 Alikufa msalabani, akililia rehema. Alikufa, akiomba maji anywe. Alikufa, akiomba rehema. Alikuwa ni Mwanadamu wakati alipokufa.

209 Lakini kwenye siku hiyo ya tatu, wakati unabii huo ulipotimizwa, “Sitaiacha nafsi Yake kuzimuni; wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu.” Pepo wote kuzimuni . . . Yeye alijitokeza na funguo za mauti, kuzimu, na kaburi. Alifufuka na kupaa Juu, na kuwapa wanadamu vipawa. Huyo alikuwa ni zaidi!

210 Kila mtu aliyewahi kuwa muhimu aliamini hilo, pia; washairi, na waandishi, na—na manabii wote kote katika wakati. Tungeweza kuwasaili baadhi yao.

211 Vipi kama ningeweza kumwita Eddie Perronet hapa usiku wa leo, ajitokeze jukwaani? Asingeweza kuuza nyimbo zake. Hakuna mtu angezinunua. Siku moja Roho Mtakatifu alimgusa, naye akanyakua kalamu yake, akaandika:

> Wote na wazisifu nguvu za Jina la Yesu!
> Malaika na wamsujudie;
> Leteni taji ya kifalme,
> Mkamvike Yeye taji kama Bwana wa wote.

212 Naam, bwana. Yeye ni Bwana wa wote. Aliamini ya kwamba Mungu alikuwa ndani Yake.

Loo, ninapomsikia mwingine akisema:

> Ninapoukagua msalaba wa ajabu
> Alipofia Mfalme wa Utukufu,
> Ninahesabu umaarufu wangu wote kuwa ni hasara tu.

Mwingine aliandika:

> Alipoishi, Yeye alinipenda; akifa, Yeye aliniokoa;
> Alipozikwa, Yeye aliziondolea mbali dhambi zangu;
> Alipofufuka, Yeye alinihesabia haki bure milele;
> Siku moja Yeye yuaja, O siku tukufu!

213 Kama ningemwita Fanny Crosby usiku wa leo, niseme, “Unafikiria nini kumhusu Yeye? Je! Yeye alikuwa ni nabii, ama alikuwa nini?” Yeye angesema hivi:

Usinipite, Ee Mwokozi mpole,
Yasikie maombi yangu manyenyekevu;
Wakati unapowaita wengine Wewe,
Usinipite.

Wewe ni Kijito cha faraja yangu yote,
Zaidi ya maisha kwangu,
Ni nani niliye naye duniani mbali na Wewe?
Ama ni nani Mbinguni ila Wewe?

214 Mungu asifiwe! Mungu alikuwa ndani ya Mwana Wake, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.

215 Mungu katika ulimwengu Wake! Mungu katika Neno Lake! Mungu ndani ya Mwana Wake! Naam, bwana. Sasa, Mungu ndani ya watu Wake!

216 Mnaamini Mungu alikuwa katika ulimwengu Wake? Mungu yuko katika Neno Lake? Mungu alikuwa ndani ya Mwana Wake? Sasa vipi kuhusu Mungu ndani ya watu Wake? Amina. Loo!

217 "Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena," alisema Yesu. "Hata hivyo ninyi mtaniona Mimi; kwa kuwa Mimi nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho, hata ukamilifu wa dahari. Nitakuwa ndani yenu, yeye yule jana, leo, na hata milele." Naam, bwana. Inatupasa kuwa watu wa aina gani?

218 Inanikumbusha juu ya hadithi moja. Hapa si muda mrefu uliopita, huko chini Kusini, tulikuwa tukinunua watumwa, watu weusi. Makaburu waliwaleta huku na kuwauza; Wadachi. Nao waliuzwa Marekani hapa kama watumwa. Ni kosa.

219 Kamwe haikukusudiwa wanadamu kuwatawala wenzao. Tuna Mungu mmoja. Rangi ya ngozi ya mtu haina uhusiano wowote na nafsi yake. Sote tumetoka kwenye damu moja. Mtu manjano anaweza kumpa mtu mweusi nyongeza ya damu, na vivyo hivyo mtu mweusi akupe wewe, mzungu. Sisi ni... Mungu, kwa mtu mmoja, aliyafanya mataifa yote, naam, bwana, kutokana na mtu mmoja. Lakini daima wameninii...Mungu alimfanya mwanadamu; mwanadamu akawafanya watumwa. Kamwe haikuwa sahihi, kwa kuanzia.

220 Walikuwa wakija huku na kuwauza, kama mnada wa magari ya mtumba. Wana nyumba hizi za mtindo wa kale na mashamba makubwa, nao wanakuja kule kuwanunua watumwa hawa. Wanunuzi wangepitia kule, madalali, kuwachukua. Siku moja dalali alipitia kwenye shamba fulani. Akasema, "Vema, una watumwa wangapi?"

Kasema, "Karibu mia tatu."

Kasema, "Ningependa kuwakagua." Akatoka nje.

221 Nao walikuwa na huzuni. Walikuwa mbali na nyumbani kwao. Wao kamwe—kamwe hawajui jinsi ya...Wanajua kamwe hawatarudi nyumbani tena. Kamwe hawamwoni

baba. Hawamwoni mama kamwe. Akina mama kamwe hawatawaona watoto wao. Lilikuwa ni jambo la kuhuzunisha. Nao wangewacharaza kwa mijeledi, kuwafanya wafanye kazi; kujaribu kuwasukuma, kuwafanya wafanye kazi.

222 Lakini, walimwona jamaa mmoja kijana pale, haikuwabidi kumcharaza. Kichwa chake kilikuwa kimeinuliwa juu, kidevu chake juu; alitembea kote, wakati wote, mahali hasa panapotakikana.

Yule dalali akasema, "Ninataka kumnunua mtumwa yule."

Mwenyewe akasema, "Lakini yeye hauzwi."

223 Akasema, "Tofauti ya mtu huyo ni nini?" Kasema, "Yeye ndiye bosi juu ya wote?"

Akasema, "La." Kasema, "Yeye ni mtumwa."

224 Kasema, "Labda wewe humlisha tofauti na uwalishavyo hao wengine."

Kasema, "Hapana. Yeye hula manchani, kama watumwa hao wengine."

225 Kasema, "Ni kitu gani kinachomfanya tofauti sana na watumwa wengine?"

226 Akasema, "Nilishangaa, pia, mpaka nilipopata kujua. Huko kwenye nchi ya wenyeji huko Afrika ambako wanatoka, baba yake ndiye mfalme wa kabila. Na ingawa yeye ni mgeni, hata hivyo anajua yeye ni mwana wa mfalme." Hiyo ndiyo tabia yake. Alitaka kutenda kama baba yake.

227 Loo, ni fedheha jinsi gani ilivyo leo hii, kwamba wanaume na wanawake wanaodai kuwa ni wana na binti za Mungu, wakiwa na asili ya Mungu ndani yao; wahudumu mimbarani, wakidai kuwa wana wa Mungu; na kukana kwamba kuna uponyaji wa Kiungu, wakikana kuna kutenda kazi kwa Roho Mtakatifu. Ni aibu jinsi gani kwa dada zetu wanaodai kwamba ni watakatifu wa Mungu, kukata nywele zao, na kuvua nguo zao, na kutenda jinsi wanavyotenda! Jinsi ilivyo fedheha kwa makanisa yetu, kuwaruhusu wanaume waliooa mara mbili ama tatu, kuwa mashemasi kwenye halmashauri na kadhalika! Ni aibu jinsi gani!

228 Inatupasa kutambua kwamba, ingawa sisi ni wageni katika ulimwengu huu, sisi ni wana na binti za Mfalme wa Mbinguni. Na sisi, tabia yetu ndani yetu, inapaswa kuwa kama Yesu Kristo, ili kwamba (Yeye) tupate kuiakisi Yake, kwa Utu Wake. Mungu yuko ndani ya watu Wake. Naam. Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote.

229 Yohana 14:12 ilisema, Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya, madhihirisho yale yale." Angalia kile tumekuwa tukiona juma hili, jinsi Yeye anavyojidhihirisha Mwenyewe kuwa Masihi, karama iliyokuwa

ndani Yake. Angeweza kuutambua moyo wako, ayatambue mawazo yao, awaambie ilikuwa ni kitu gani.

230 Maskini mwanamke mmoja alijisukumiza kwenye umati wakati mmoja, akagusa upindo wa vazi Lake. Akasema, "Kama itanibidi tu kumgusa Yeye!" Akakimbia akaingia kwenye umati, akasimama, akaketi chini, chochote kilichokuwa.

231 Huku kila mtu anamkumbatia Yeye, "Aloo, Rabi, Nabii kijana! Unaendeleaje?"

232 Na baadhi yao wakisema, "Hei, ninasikia unaweza kuwafufua wafu! Tuna makaburi yaliyojaa hao." Wakosoaji, unawapata tu kila mahali.

233 Naye Huyo hapo, akijisukumiza. Baada ya kitambo kidogo akasimama. Akasema, "Ni nani aliyenigusa Mimi?"

234 Wakati, huenda Petro alisema maneno haya, "Bwana, watadhani kuna kasoro fulani ya kiakili. Angalia mikono na viganja vinavyokugusa Wewe kutoka kila mahali, na halafu unasema, 'Ni nani aliyenigusa Mimi?'" Alimkemea kwa ajili ya hilo.

235 Yesu akasema, "Lakini nilihisi mguso tofauti, mguso halisi."

236 Wengi sana wetu usiku wa leo wana maungamo, wengi sana wetu wanafanya mambo mbalimbali, lakini hata hivyo kuna mguso, kuna kitu ambacho huvutia usikivu wa Mungu. Naye Mungu hujiakisi Mwenyewe ndani ya mtoto Wake. Kazi afanyayo Yeye, tunapaswa kufanya hiyo hiyo.

237 Pale maskini mwanamke huyo ameketi chini. Yesu aliangalia kote hata akampata. Alimwambia kuhusu kutokwa kwake na damu, na kusema imani yake ilikuwa imemwokoa.

238 Loo, tunamwona Yeye wakati maskini yule mwanamke, pale kisimani, anakuja kuchota ndoo ya maji. Naye alikuwa na kiu, ndipo akaanza kuitelemsha ndo—ndoo humo kisimani, wakati alipomsikia Myahudi kijana akisema, "Nipe maji ninywe."

239 Akaangalia kule akasema, "Si kawaida. Tuna ubaguzi hapa. Hupaswi kuniomba mimi, mwanamke."

240 Kasema, "Lakini kama ulijua ni Nani ulikuwa ukizungumza naye, ungeniomba Mimi maji unywe." Ndipo basi akaendelea na mazungumzo mpaka akajua kilichokuwa shida yake. Akasema, "Nenda kamwite mume wako mje hapa."

Akasema, "Sina mume."

241 Akasema, "Umesema kweli. Unao watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako. Umesema kweli."

242 Akasema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii. Nasi tunajua kwamba ajapo Masihi, hili ndilo jambo hasa atakalofanya."

243 Akasema, "Mimi ninayesema nawe Ndiye." Loo, jamani! Alikuwa akifanya nini? Akimwakisi Mungu.

244 Kanisa linapaswa kufanya nini? Kuakisi jambo lile lile alilofanya Yeye. Hakika. Loo, kuakisi, Mungu ndani ya watu Wake!

245 Ninakumbuka, katika Biblia, wakati nabii wa kale, aliyejazwa sana na Roho Mtakatifu, mpaka mwanamke Mshunami akapata mtoto mchanga. Kisha akafa, naye nabii hakuninii, asingeweza kusikia kutoka kwa Mungu, mahali popote. Bali alitembea huku na huku sakafuni, huku na huku, mpaka Roho wa Mungu akaja juu yake. Akajinyosha juu ya maskini mtoto huyo aliyekufa, naye akapiga chafya mara saba, akafufuka. Ilikuwa ni kitu gani? Huyo nabii? La, bwana. Mungu ndani ya watu Wake. Hiyo ni kweli. Ilikuwa ni Mungu ndani ya watu Wake. Hakika. Hiyo ni kweli kabisa.

246 Tunamwona mtu jina lake Mtakatifu Petro, hakuwa na elimu ya kutosha, hana ujuzi wa seminari, hakuwa na kadi ya ushirika kutoka kwa shirika lolote. Bali alijazwa na Roho Mtakatifu, Mungu ndani ya watu Wake. Walimwona akitabiri, na kuona ikitimia. Waliyaangalia maisha yake makuu. Walisikia ushawishi wake. Mtu, yeye alinena kama Yesu Kristo. Biblia ilisema, ya kwamba, "Walitambua walikuwa watu wasio na elimu wala maarifa, bali walijua walikuwa pamoja na Yesu." Mnaona? Mnaona? Linajiakisi Lenyewe ndani yako. Nao wanaona, hao watu waliamini sana, sana, Mungu akaja juu ya watu hao, hata wakalala chini ya kivuli cha huyo mvuvi wa samaki asiye na elimu. Na wote waliolala hapo, wakiwa na imani, wakiamini, waliponywa. Si kivuli cha huyo mvuvi, bali Mungu ndani ya watu Wake, Mungu akitenda kazi kupitia watu Wake. Hakika.

247 Walimwona Paulo akisimama pale na kutoa unabii. Na kila mmoja ukatimia kikamilifu; kutabiri mambo, na kufanya kila kitu ambacho Yesu Kristo alifanya wakati Yeye alipokuwa hapa duniani. Waliona ya kwamba yeye alikuwa pamoja na Kristo. Wanajua Kristo alikuwa pamoja naye, mpaka hata wakamtaka achukue leso na nguo kutoka mwilini mwake, nao wakaviweka juu ya wagonjwa na wanaoteseka, nao pepo wachafu wakawatoka watu hao. Magonjwa yaliponywa. Ni kitu gani? Mungu ndani ya watu Wake.

248 Loo, kile tunachohitaji usiku wa leo! Hebu angalia jana usiku. Nilikuwa nikisikiliza kanda. Maskini mwanamke mmoja alishuka akaja kutoka, ninaamini, Oregon, ama mahali fulani. Alikuwa ni mwanamke maskini. Alikuwa ametumia fedha zake kuja hapa. Alikuwa na mume asiyeokoka na watoto. Alikuwa mgonjwa na anayeteseka, akaja jukwaani. Mtu fulani huko nje aliwazia jambo tofauti, kwamba nilikuwa nikibahatisha shida aliyoambiwa kuwa anayo.

249 Ndipo Roho Mtakatifu akarudi nyuma na kumwambia kwamba yeye alikuwa ni nani, jina lake lilikuwa ni nani, na

alivyoitwa na mama yake. Akamwambia hapo alipokuwa mtoto mchanga, lile jina lake, alilopewa. Akamwambia jina lake la ndoa lilikuwa ni nani sasa. Akamwambia mahali alipokuwa, yale aliyokuwa ametenda, alikotoka, yale aliyokuwa akifanya, ugonjwa aliokuwa nao. Na kusema alikuwa na mume mwenye dhambi, na—na watoto wenye dhambi, naye alikuwa akiugua ugonjwa wa namna fulani. Sijui sasa. Nilisikiliza tu kanda hiyo.

250 Ndipo Roho Mtakatifu akaja na BWANA ASEMA HIVI. "Ninakupa mume wako. Ninakupa watoto wako. Ninakuponya." Na leo hii yeye ni mzima. Mume wake alikuwa ndiye wa kwanza madhabahuni, jana usiku, nao watoto wake wameokoka.

251 Ni kitu gani? Yeye anayejua wakati uliopita, wakati uliopo, wakati ujao. Ni kitu gani? Mungu ndani ya watu Wake. Amina. Hiyo ni kweli. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye aliahidi mambo haya katika siku za mwisho.

252 Mimi huyu hapa, nimemaliza, saa nne kasoro dakika kumi. Samahani, mimi ninaendelea tu kuzungumza. Nina Maandiko mengine thelathini yaliyowekwa hapa. Loo, loo! Nitayahifadhi kwa ajili ya kesho usiku.

253 Mungu ndani ya watu Wake. Mnaamini Mungu yuko katika ulimwengu Wake? Mnaamini Mungu yuko katika Neno Lake? Mungu yuko ndani ya Mwana Wake? Mungu ndani ya watu Wake? Hivi hamna furaha kujua ya kwamba Mungu yuko katika ulimwengu, Mungu yuko ndani ya Mwana Wake, Mungu yuko ndani ya watu? Mungu angali ni Mungu. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Jina la Bwana libarikiwe! Nawaambia.

Na tuombe. Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

254 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuamini Wewe kuwa ni Mungu. Tunajua kwamba Wewe u karibu. Tunakuona Wewe huko nyuma kabla ulimwengu haujaanza. Tunakuona Wewe ukiinyosha mikono Yako, ukaufanya ulimwengu. Ulimwengu umewekwa pamoja kwa Neno la Mungu. Mavumbi yenyewe tuliyoketi juu yake usiku wa leo ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Kama sivyo, yalitoka wapi? Ulinena, yakawa. Wewe ungali ni Mungu, usiku wa leo. Ee Mungu, tujalie sisi—tujalie sisi tuone ono lake. Jalia tushike maana halisi ya Neno Lako la thamani. Tujalie, Baba. Tubariki usiku wa leo.

255 Ninaomba ya kwamba Wewe utatujalia usiku wa leo, ya kwamba Wewe utaonyesha ya kwamba Wewe uko ndani ya watu Wako. Sasa, wanaweza kukuona Wewe katika ulimwengu. Wanaweza kukuona mahali mbalimbali, Bwana. Sasa tujalie—tujalie tukuone Wewe ukijitokeza, Baba yetu wa Mbinguni, kama itatupa hisani. Ninaomba kwamba Wewe utaona, Bwana, kwamba hatumaanishi kwamba ni lazima tuyaone mambo haya, bali ili kwamba Neno Lako lipate kutimizwa. Hukuhitaji kuwaponya watu, kuthibitisha Wewe ulikuwa Mwana wa Mungu. Ulifanya hivyo kwa sababu ulisema ilikuwa ili kwamba

Neno litimizwe. Na usiku wa leo, Wewe hufanyi mambo haya kwa sababu tu unafikiri unapaswa kuyafanya. Unayafanya kwa sababu umeahidi kuyafanya. Wewe u—unawajibika kwa Neno, Bwana, na hakika Wewe daima unalifanya kweli.

256 Hizi hapa leso zimewekwa hapa, Bwana, za watu wagonjwa. Kotekote nchini, kunao maskini watoto wagonjwa, akina mama. Umeziona leso hizi. Ninaweka mikono yangu juu yazo, Baba. Ninajua mimi si Mtakatifu Paulo, bali Wewe ungali Yesu.

257 Pia ilisemwa wakati mmoja, katika Biblia, ya kwamba kundi la watu, walioitwa Israeli, walikuwa wakitii amri Yako. Walikuwa wakitembea moja kwa moja kwenye barabara ya wajibu wao. Na wakisimama kwenye jukumu lao, Bahari ya Shamu ikawazuia. Ikawakatilia mbali. Jeshi la Farao lilikuwa likikaribia. Milima na majangwa yalikuwa pande zote mbili. Ilionekana kana kwamba Mungu hakujiachia Mwenyewe mahali pa kurudi nyuma, bali kulikuwako na kitu fulani njiani. Uliwaahidi ya kwamba Wewe ungewapeleka kwenye nchi mpya. Bahari ya Shamu ikawazuia. Mwandishi mmoja alisema, ya kwamba, "Mungu aliangalia chini kupitia hiyo Nguzo ya Moto, kwa macho yenye hasira." Kasema, "Wakati Yeye alipofanya hivyo, Bahari ya Shamu ikaogopa, nayo ikarudi nyuma, nao Israeli wakaendelea na safari."

258 Ee Mungu wa Mbinguni, Wewe ungali ni Yehova usiku wa leo. Sio tu kuangalia kupitia Nguzo ya Moto, bali angalia chini kupitia Damu ya Mwana Wako Mwenyewe usiku wa leo. Nao ugonjwa umewazuia watu hawa wagonjwa hapa, ambao leso hizi zinawawakilisha. Yehova Mungu mkuu, leso hizi zitakapowekwa juu ya wagonjwa, jalia ibilisi huyo aogope, arudi nyuma. Mungu, wapeleke kwenye ile ahadi, "Mimi ni Bwana ayaponyaye magonjwa yenu yote." Tujalie, Baba. Katika Jina la Mwana Wako, Yesu Kristo, tunaomba.

259 Na sasa, Bwana, wabariki wanaongojea katika kusanyiko. Ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

260 Sasa, ninaamini tumechelewa kidogo tu. Tumekuwa tukiita kadi za maombi kila usiku, kuja huku madhabahuni. Ninaamini tutawaita tu wale wasio na kadi za maombi usiku wa leo, kusudi muone ya kwamba kadi ya maombi haina uhusiano wowote nalo. Ni wangapi hapa ndani walio wagonjwa na hawana kadi ya maombi? Inua mkono wako. Vema. Hakuna mtu hapa, ninayemwona, ambaye ninamjua. Siwezi kumtaja mtu mmoja, ila tu maskini waimbaji hawa wanaoketi hapa mbele.

261 Kama nilisema Mungu yuko katika ulimwengu Wake, Mungu yuko ndani ya watu Wake. Mnaamini Mungu yuko ndani ya watu Wake?

262 Sasa, kila mmoja wenu, angalia upande huu. Kama Petro na Yohana walivyosema, walipopitia kwenye lango liitwalo Zuri, walisema, "Tutazame sisi." Hilo linamaanisha, "Kuzingatia.

Sikiliza yale nitakayosema." Akasema, "Sina fedha wala dhahabu. Lakini nilicho nacho, kama imani; nilicho nacho, nakupa wewe. Katika Jina la Yesu Kristo, simama." Akanyosha mkono akamshika, mtu huyo, akaanza kumshikilia asimame, mpaka mifupa ya kifundo cha mguu wake ikapata nguvu. Ndipo akaondoka, akishangilia.

263 Kama mnavyojua tayari, mimi sina elimu. Sina. Nisingeweza kujiita mhubiri. Kwa namna fulani mimi ni tairi ya akiba. Ila Mungu alinipa karama, kama karama ya kumdhihirisha Yesu Kristo, kuwafanya watu waone kwamba Yeye angali anaishi. Sasa, iwapo . . .

264 Yeye hajafa. Kama amekufa, basi dini ye—yetu ni bure. Lakini nimeona mamia ya dini, kama mmishenari kote ulimwenguni, nikikabiliana na kila namna ya pepo, waganga, na kila kitu. Lakini dini yetu ni ya kweli. Mungu wetu anaishi. Hajafa. Yu hai. Na Yeye aliahidi, "Kazi nizifanyazo Mimi nanyi pia mtazifanya."

265 Nawaambia, kwamba, mtu yeyote ambaye amezikiri dhambi zake, na chini ya Damu ya Yesu Kristo, yeye ni mwana wa Mungu, kama amezaliwa kwa Roho wa Mungu. Hao ni wana na binti za Mungu.

266 Sasa, vipi kama Yesu alikuwa amesimama hapa usiku wa leo, amevaa suti hii ambayo Yeye alinipa mimi kupitia rafiki yangu mwema, Carl Williams? Vipi kama—kama Yeye alikuwa amesimama hapa na amevaa suti hii, nawe ungeenda Kwake, useme, "Bwana Yesu, utaniponya?" Mbona, asingeweza kufanya hivyo. Tayari amefanya hilo; kwa mapigo Yake sisi tuliponywa. Ungesema, "Nisamehe." Alifanya hilo pale Kalvari. Kazi hiyo ilikamilika, ya mpango wote wa wokovu. Uponyaji na yote yalikamilika.

267 Biblia ilisema, ya kwamba, "Alipaa Juu, ameketi mkono wa kuume wa Mungu." Mnaamini hilo? Yeye yuko kule kufanya uombezi, na Yeye ni Kuhani wetu Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Mnaamini hilo? "Mwombezi wetu wa pekee kati ya Mungu na wanadamu ni Yesu Kristo." Hiyo ni kulingana na Biblia. Huenda ukawa na wengine wakijaribu hilo. Bali kuna Mmoja tu ambaye Mungu humsikia, na huyo ni Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Angalia, wakati Yeye ameketi pale, Kuhani Mkuu, yeye yule jana, leo, na hata milele.

268 Sasa, kama alikuwa akitembea hapa usiku wa leo, nawe ulikuwa na imani ya kuamini ya kwamba Yeye angeweza kukuponya, kama tu maskini mwanamke yule aliyeamini ya kwamba Mungu alikuwa ndani ya Mwana Wake! Sasa, mnaamini ya kwamba Mungu yuko katika Neno Lake. Mnaamini Mungu yuko ndani ya watu Wake.

269 Yesu alifufuka kutoka kwa wafu, akarudi kuwa Roho Mtakatifu, ndipo akarudi tena, akiishi ndani ya watu Wake,

kufanya kazi zile zile alizofanya Yeye. Nayo saa imekaribia kwa ajili ya hili kutimizwa, maana mwisho wa kipindi cha wakati wa Mataifa umekaribia. Alililifanya mwishoni mwa cha Kiyahudi, mwisho wa cha Kisamaria, na sasa mwishoni mwa cha Kimataifa, kama tu alivyofanya wakati huo. Aliahidi kufanya hilo, kulingana na Maandiko.

Sasa, kila mmoja wenu huko nje, aliye mgonjwa na mhitaji . . .

270 Naye Baba wa Mbinguni anajua ninasema ukweli. Kama kuna mtu yeyote ninayeweza kumwona katika jengo hili, ambaye ninamjua, kwenye wakati huu, akiangalia huku, ni hawa wavulana wadogo wanaoketi papa hapa, na msichana mdogo, aliyeimba, ndio tu ninaoona, ambao ninawajua.

271 Ni wangapi wenu huko nje ambao wanajua sijui lolote kuwahusu, ninyi ni wageni? Inua mkono wako. Mnaona? Kila mtu. Sijali mahali ulipo, huko nyuma, popote pale.

272 Sasa, kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na Yeye ni Kuhani Mkuu, nasi tunakuwa kituo cha kupokelea Kwake. Kazi alizofanya Yeye, tunapaswa kuzifanya pia. Ninajua mnaweza kusikia mahubiri ya kisaikolojia. Tunaweza kuzungumzia kile Yeye alichokuwa, na, mbona, hilo ni sawa. Lakini je! itafanya kazi? Tunaweza kusema Yeye ni yule yule, lakini je! itafanya kazi? Kama mtu akijaribu kuuza kitu fulani; kinaonekana kizuri, bali hebu tukione kikifanya kazi.

273 Sasa, dini yetu haina budi kuwa katika matendo. Dini ya Kikristo ni matendo. Ni Yesu Kristo Mwenyewe, katika matendo, awezaye.

274 Ni kama tu maikrofoni hii hapa, maikrofoni hiyo ni bubu kabisa mpaka kitu fulani kizungumze kwake. Ndipo inapeleka sauti ya kile kilichozungumza ndani yake. Lakini, yenyewe, ni bubu.

275 Na vivyo hivyo mwanamume yeyote ama mwanamke. Wewe ni bubu inapofikia mambo haya, bali ukiwa katika mawasiliano, naye Kristo amekuvuta huku apate kukutumia, sio wewe. Siyo sauti yako. Ni Yake.

276 Hiyo ndiyo sababu nitamshuhudia mtu yeyote, katika makumi elfu mara maelfu ya nyakati, mlipata kuiona ikikosea? Kamwe haitakosea, kwa sababu ni Mungu.

277 Sasa, huna budi kuliamini. Huna budi kulikubali. Huna budi kuwa na imani, na usilitilie shaka.

278 Sasa, kwenu ninyi huko nje kwenye wasikilizaji, ninawatakeni mwinamishe vichwa vyenu kwa dakika chache, nami nawatakeni mwombe kama maskini mwanamke yule alivyofanya. “Bwana, mimi ni mgonjwa.” Ama, “Nina rafiki mgonjwa.” Ama, “Nina hitaji, kubwa. Nina matatizo ya kinyumbani,” ama chochote kile ulicho na haja nacho.

279 Useme, “Bwana Yesu, ninajua mtu huyo hanijui mimi. Yeye ni mgeni kabisa kwangu mimi. Lakini, Wewe unanijua. Nami ninakutaka Wewe, Baba wa Mbinguni, unisaidie. Ninakutaka Wewe u—uniponye. Nami ninaenda kugusa vazi Lako. Niko mbali sana naye, isingefaa kitu kumgusa, hata hivyo; yeye ni mwanadamu tu. Ila ninaenda kukugusa Wewe. Naye ametwambia ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho, nayo ishara ya mwisho imeligusa kanisa; kulingana na Maandiko, kama vile Wewe ulivyomjia Ibrahimu, yule mteule aliyeitwa kutoka Sodoma. Sasa, Baba Mungu, na iwe, usiku wa leo. Jalia tu iwe, Baba, ya kwamba wakati. . .Jalia mtu huyu aniambie, aseme nami kama Yeye alivyosema na mwanamke aliyegusa vazi Lake, nami nitakuamini Wewe kwa moyo wangu wote.”

Sasa acha muziki uwe kimya kabisa, tafadhali, bwana.

280 Sasa ombeni. Sasa, kila mtu aliye mgonjwa, mtu yeyote asisogee. Wala msi—msininii. . .

281 Mtu fulani ndiyo kwanza apige picha. Usipige tena. Unaona, Roho Mtakatifu ni Nuru. Ninaiangalia.

282 Sasa mnaona mahali ninaposimama? Hili hapa kundi la wahudumu wa—wafadhili nyuma yangu. Kuna yapata watu elfu moja wanaoketi mbele yangu. Wakati, nimeona wakati ambapo nusu milioni wameketi pale. Simjui hata mtu mmoja.

283 Nanyi, usiku wa leo, msio na kadi za maombi, ninawatakeni muombe tu na kusema, “Bwana Yesu, jalia huu uondolewe, ushirikina wote, kutoka kwangu. Yeye alisema Mungu alikuwa ndani ya watu Wake. Alisema kwamba Mungu alikuwa amemtuma kumtangaza Yesu Kristo katika siku za mwisho, kwa Kanisa. Mimi ni mgonjwa. Basi laiti ningaliweza tu kugusa vazi Lako, usiku wa leo! Hao, wananiambia Biblia hunena na kusema, ‘Wewe ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.’ Nayo Biblia ilisema, ‘Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele.’ Basi, ungetenda leo kama ulivyotenda jana. Na yule mwanamke alikugusa Wewe, kisha akaketi chini katika kusanyiko, na Wewe ukageuka na kumwambia kilichokuwa shida yake, na ukasema imani yake ilikuwa imemponya.”

284 Sasa omba kwa uaminifu, na Bwana Mungu na aijalie haja hiyo, ndilo ombi langu. Sasa iweni tu na kicho kabisa. Ombeni kwa dakika moja tu. Iwapo wewe ni mwenye dhambi, sema, “Nisamehe, Bwana.” Kama wewe ni mgonjwa, na mwenye dhambi, sema, “Nisamehe, Bwana.” Kama wewe ni Mkristo, una haki kwenye Mti wa Uzima.

285 Sasa, kama unajisikia kama kwamba umeomba, nawe una jambo fulani, ambalo, sasa iweke tu nia yako juu ya Kristo. Unaweza kuinua kichwa chako ukitaka, na uiweke tu nia yako juu ya Kristo, na uangalie huku. Angalieni huku, kuelekea kwangu.

286 Na sasa amini tu kwa moyo wako wote, useme, "Bwana Yesu, vizuri zaidi nijuavyo, nimeomba maombi ya imani. Na sina kadi ya maombi. Sitaitwa kwenye mstari wa maombi. Ama, kama akiitisha mstari wa maombi, baada ya kitambo kidogo, sitakuwa hapo. Sina kadi ya maombi. Lakini ni—nina imani, Mungu. Nisaidie."

287 Sasa wewe fanya hivyo. Halafu basi ikiwa Yesu Kristo atashuka na kututia upako, imani yako kuliamini, macho yangu kuliona, na midomo yangu kulinena! Na kama Yeye akifanya jambo lile lile alilofanya jana wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, na akaahidi kulifanya tena, basi Mungu yuko ndani ya watu Wake. Ndipo unasema, "Utuonyeshe Baba, na hilo litatutosha."

288 Omba tu. Sasa, si imani yangu. Ni yako. Mimi ninamngojea tu Yeye aseme nami. Asiponena, basi nitaitisha mstari wa maombi. Hayo ndiyo yote niwezayo kufanya. Sasa, si—sijiwezi bila Yeye. Bali nina hakika Yeye yupo hapa. Kabisa. Laiti ningaliweza tu kumwona mtu fulani aliye na imani! Msiwe, msiwe na wasiwasi. Kamwe hupati chochote, kwa kuwa na wasiwasi. Kwa uchaji tu, mbele za Mungu, wasilisha tu haja zako.

289 Ni wakati wa jinsi gani! Ni wakati wa jinsi gani! Mnaona? Mungu, Neno, ni Kweli, nalo Neno litapatikana. Ama mimi ni shahidi wa uongo wa Neno, au, kama nimesema Kweli, Mungu atathibitisha Neno hilo ni Kweli. Hiyo ni kweli. Mungu hatakuwa na uhusiano wowote na uongo. Mnajua hilo.

290 Huyu hapa. Asante, Bwana. Katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho humu ndani, chini ya udhibiti wangu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

291 Aminini sasa, kwa uchaji, na muamini. Yule Malaika mnayemwona katika ile picha, yupo hapa jukwaani. Anaingia katika kusanyiko. Hebu kidogo. Ameondoka . . .

292 Hii hapa. Mnaweza kuiona Hiyo? Ni maskini mama anayeketi papa hapa nje, karibu mwishoni mwa safu. Mnaiona ile Nuru, kaharabu, papo hapo karibu na mama huyo? Yuko karibu kujifungua. Si hiyo ni kweli? Una kadi ya maombi? Huna. Huhitaji moja. Lakini ulikuwa unaamini. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, mtumishi Wake? Kama Bwana Yesu Kristo atanifunulia mambo yaliyo moyoni mwako, na kile kilichokuleta hapa, utalikubali?

293 Una wasiwasi, bila shaka, ukijiandaa kujifungua, bali shida yako iko mgongoni mwako. Una shida mgongoni mwako, na hiyo ndiyo hasa ulikuwa ukimwomba Mungu akuponye. Hiyo si ni kweli? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa, ikiwa mambo hayo ni kweli, yale ambayo yamesemwa ni kweli, ninataka usimame ili kwamba watu wajue ni kweli. Sisi ni wageni kabisa mmoja kwa mwingine? Kama hiyo ni kweli, inua

mkono wako. Je! yale Yeye aliyosema ni kweli? Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako namna *hii*.

294 Sasa, huyo hapo mwanamke aliyegusa vazi Lake. Asingeweza kunigusa. Yuko futi thelathini ama arobaini kutoka kwangu. Bali aliligusa vazi Lake. Basi mwulizeni. Amekuwa akiomba ya kwamba Mungu auponye mgongo wake na amjalie kumzaa mtoto huyo mchanga. Hiyo ni kweli. Je! hiyo ni kweli? Na ulifanya hivyo kabla hujaja hapa kanisani usiku wa leo, na ukaomba ya kwamba kwa njia fulani utaruhusiwa kwenye mstari wa maombi. Ikiwa hiyo ni kweli, ikiwa hilo ndilo ombi lako, inua mkono wako. Ninawezaje kusimama hapa na kumwambia yale aliyosema kabla hajatoka nyumbani? Unaamini Mungu anaweza kuniambia jina lako ni nani? Bibi Cisco. Amini kwa ninii yote. . .Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako. Sasa nenda nyumbani. Umepona. Mungu akubariki pamoja na mtoto huyo, na mume wako aliyeketi hapo.

295 Mbele za Mungu, sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu hapo kabla. Je! Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele?

296 Hapa, maskini mwanamke anayeketi pale, anayeonekana kama Mhispaniola. Alisisimkwa sana juu yake. Anatambua jambo fulani linaendelea. Analia kwa sababu hiyo Nuru iko moja kwa moja juu yake. Simjui. Sijawahi kumwona. Bali alikuwa na kitu fulani moyoni mwake, alichokuwa akiombea. Ni kuhusu mama yake. Hiyo ni kweli. Una kadi ya maombi? Huhitaji moja. Huna yoyote. Huhitaji moja.

297 Mama yako, ni mgonjwa sana. Hayupo hapa. Yuko Bakersfield. Hiyo ni kweli. Wewe ni mke wa mhudumu. Huyo aliyeketi karibu na wewe ni mume wako. Anaye kaka. Humwita "Joe." Hiyo ni kweli. Sasa, kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sijawahi kuwaona watu hao maishani mwangu. Kama hiyo ni kweli, ninyi wawili simameni kwa miguu yenu. Kama hiyo ni kweli, nami ni mgeni kabisa kwenu, inueni ninii yenu. . .Mmepokea haja yenu. Nendeni nyumbani. Yesu Kristo amewasikia. Mungu asifiwe!

298 Huyo mwanamke aliyeketi papo hapo nyuma, aliyevaa blauzi hiyo inayoonekana ya waridi, una kadi ya maombi, mama? Mimi ni mgeni kwako. Sikujui. Je! hiyo ni kweli? Lakini kuna duara nyeusi, inayoonekana gizagiza, inayomzunguka-zunguka mama huyo. Ina maana gani? Bwana Mungu na aniambie. Naam, ninamwona akianguka. Ana namna fulani ya mpagao. Ana kifafa. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaamini Yesu Kristo anaweza kukuponya? Basi ukubali uponyaji wako. Naomba usiwe na mwingine, katika Jina la Yesu Kristo.

299 Unaamini kwa moyo wako wote? Iweni na imani katika Mungu. Mnaamini? Angalieni. Huyu hapa tena. Angalieni.

Iko juu ya maskini mwanamke mmoja, mwanamke mdogo, anayeonekana amekonda, anayeketi papa hapa chini. Anaugua ugonjwa wa u—u—upungufu wa damu. Ataukosa.

300 Bwana Mungu, nisaidie. Tafadhali, naomba, Baba, usiruhusu impite.

301 Jina lake ni Bibi Marsh. Simama, Bibi Marsh, na ukaponywe, katika Jina la Yesu Kristo.

302 Shetani alidhani angepita na hilo, bali alilikosa. Simjui mwanamke huyo. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Mungu Mbinguni anajua.

303 Ni kitu gani? Mungu katika ulimwengu Wake, Mungu katika Neno Lake, Mungu ndani ya Mwana Wake, Mungu ndani ya watu Wake. "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Mnaamini, kwa moyo wenu wote? Ni wangapi wanaliamini? Inueni mikono yenu.

304 Ni wangapi wanaomhitaji Mungu maishani mwako? Inueni mikono yenu na mpunge mikono yenu.

305 Sasa ichukueni mikono hiyo inayopungwa, na muwekeane ninyi kwa ninyi, nami nitawaombea kutoka hapa. Wewe mwombee mtu fulani. Wekeaneni mikono nanyi mtauona utukufu wa Mungu. Sijali jinsi ulivyolemaa. Kama kuna mtu yeyote hapa kwenye kiti cha magurudumu, mtu yeyote kwenye mikongojo, mtu yeyote asiyeweza kutembea, jiandae, utatembea. Utatembea ukitoka, kama ukiamini. Wekeaneni mikono mmoja na mwenzake, na mwombeane. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yupo hapa, Mungu ndani ya watu Wake. Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

306 Baba wa Mbinguni, ninakuja kuomba neema isameheayo na maombi kwa ajili ya watu hawa, wakati tukijua ya kwamba Uwepo Wako upo hapa. Naomba ya kwamba kila nguvu za ibilisi zivunjwe, katika kusanyiko hili, na kwamba Yesu Kristo atautwaa mkutano huu wakati huu, na atamponya kila mgonjwa aliye kwenye Uwepo wa Kiungu. Kupitia Jina ya Yesu Kristo naomba.

307 Ninaamini hilo. Sijali una shida gani, shida ambayo imekuwepo. Nitakutangaza "umeponywa." Kama unaamini, kwa moyo wako wote, acha mikongojo yako ikae mahali ilipo. Ambapo ninii yako. . . Shida iwayo yote, simama kwa miguu yako na ushuhudie kwa Mungu kwamba unakubali uponyaji wako kwenye wakati huu. Simama kwa miguu yako. Na uamini kwa moyo wako wote ya kwamba Yesu Kristo. . . Haya basi. Jambo ndilo hilo. Kundi zima linasimama, asilimia mia moja. Yesu Kristo amemponya kila mtu aliye katika Uwepo wa Kiungu, ambaye ameamini.

308 Sasa, iwapo humjui Yeye kama Mwokozi wako, njoo hapa sasa ukampokee wakati Uwepo Wake ukiwa hapa. Utatembea kuja hapa sasa na kumpokea? Inueni mikono yenu kwa Mungu na mumpe shukrani na sifa, wakati nikimwomba mmoja wa wachungaji kama ataichukua ibada.

Njoo hapa. Mungu akubariki, ndugu.

63-0606 Utuonyeshe Baba
Ramada Inn
Tucson, Arizona Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org